# JARIDA
## LA CHAMA CHA MAPINDUZI


MIAKA KUMI NA MOJA YA TAWI
2014
2025

# TAWI LA CCM CHINA

*"Hauhitaji Kuwa Mkomunisti kutambua kwamba China ina mambo mengi ya kutufundisha kuhusu maendeleo..."*

~Julius Kambarage Nyerere





# JARIDA LA CHAMA CHA MAPINDUZI TAWI LA CHINA

1

TOLEO LA KWANZA

# YALIYOMO


- **SEHEMU YA KWANZA.** 11-18
  *Historia ya Tawi la CCM China.*
- **SEHEMU YA PILI.** 19-31
  *Viongozi wakuu wa CCM toka  kuanzishwa kwake.*
- **SEHEMU YA TATU.** 32-45
  *Uhusiano wa Tanzania na China mtazamo wa kihistora.*
- **SEHEMU YA NNE.** 46-51
  *CCM na ajenda za maendeleo.*
- **SEHEMU YA TANO.** 52-76
  *Vivutio na utalii nchini Tanzania.*
- **SEHEMU YA SITA** 77-83
  *Fursa za uwekezaji Tanzania.*
- **SEHEMU YA SABA** 84-90
  *Fursa za elimu zinazopatikana katika jamuhuri ya watu wa China.*

# Dibaji Kutoka Kwa Mwenyekiti wa Tawi la CCM China

## Cde.
## Hussein Ally Kanduru



### Kidumu Chama Cha Mapinduzi.

Kwa moyo wa dhati na kwa heshima kubwa, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha kwenye toleo la kwanza la Jarida la Chama Cha Mapinduzi Tawi la China.

Hili ni chapisho maalum linalolenga kuangazia historia fupi ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na harakati za Tawi letu la China, huku likielezea masuala muhimu ya uhusiano wa kimataifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China.

Katika jarida hili, tumegusia maeneo mbalimbali kama vile: maendeleo ya kijamii na kiuchumi, sekta ya utalii, fursa za elimu zinazopatikana kati ya mataifa haya mawili, pamoja na fursa za uwekezaji katika sekta za kimkakati. Katika enzi hizi za mabadiliko ya kidijitali, dhamira yetu kama tawi ni kutumia vyema teknolojia na mitandao ya mawasiliano kuwasilisha taarifa sahihi, zenye mtazamo chanya, fikra pevu na zenye kuakisi uhalisia wa maisha ya Watanzania na mchango wa CCM katika kuyaleta maendeleo.

Sisi ni vijana wa kizazi kipya, wenye ari, nguvu, na dhamira ya kweli ya uongozi. Tunaamini kuwa siasa ni nyenzo muhimu ya kuleta mabadiliko chanya, kujenga kesho yenye

matumaini, amani, na maendeleo kwa kila Mtanzania. Tunaamini kuwa maamuzi ya busara yanayofanywa na viongozi wetu, kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu, yana uwezo wa kuathiri kizazi cha sasa na kijacho kwa namna chanya na endelevu.

Kwa msingi huo, Tawi letu limejikita katika kuanzisha jukwaa la maarifa lenye taarifa sahihi kuhusu maendeleo, changamoto na fursa zilizopo nchini Tanzania. Tunatambua kuwa taarifa ni nguvu, na propaganda nzuri ni silaha ya kuhamasisha fikra chanya, mshikamano na mapenzi kwa taifa.

Mwaka 2025 ni mwaka muhimu kwa taifa letu, ambapo tumeshiriki katika Uchaguzi Mkuu. Katika muktadha huu, jarida hili litaeleza kwa kina sababu za msingi zinazofanya Chama Cha Mapinduzi kuendelea kuwa chaguo sahihi kwa Watanzania. CCM imeonesha uwezo mkubwa katika uongozi tangu enzi za harakati za uhuru hadi sasa, ikitekeleza kwa mafanikio makubwa sera zake na kusimamia rasilimali za nchi kwa manufaa ya wananchi wote.

Tunatambua kuwa wasomaji wetu watakuwa na mitazamo na fikra mbalimbali kuhusu siasa. Hivyo basi, lengo letu si kushawishi kiholela, bali ni kuelimisha, kuhamasisha, na kuibua mijadala yenye kujenga, ili kila Mtanzania awe na uwezo wa kufanya maamuzi kwa kutumia taarifa sahihi. Tunaheshimu uhuru wa fikra na tunaamini kuwa taifa hujengwa juu ya msingi wa maarifa na mshikamano.



Kama Mwenyekiti wa CCM – Tawi la China, nawakaribisha kwa mikono miwili katika jarida letu. Tunaamini kuwa siasa si mchezo wa watazamaji, bali ni uwanja wa ushiriki, mjadala na ubadilishanaji wa fikra. Huu ni mwanzo wa safari mpya ya kusambaza misingi, sera na maono ya Chama Cha Mapinduzi kwa Watanzania walioko nje ya mipaka ya nchi, ili kuendeleza mshikamano ndani ya chama na taifa kwa ujumla.

Tunathamini sana maoni, ushauri na mrejesho kutoka kwenu baada ya kusoma jarida hili. Hayo yatatusaidia kuboresha machapisho yajayo, kwa sababu msingi wa siasa bora ni KUSIKILIZA, KUTENDA, na KUBORESHA.

Asanteni kwa kuchagua Jarida la CCM-CHINA kama chanzo chenu cha kuaminika cha maarifa ya kisiasa.

**Kidumu Chama Cha Mapinduzi.**

# Ujumbe kutoka kwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katika Jamhuri ya watu wa China.

## Mhe. **Khamis Mussa Omar**

### Makomredi, Kidumu Chama Cha Mapinduzi.

Urafiki wa kidugu baina ya Jamhuri ya Muunganio wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China uliasisiwa na dhamira ya ukombozi – wa uhuru, utu, na kujiamulia mambo yetu wenyewe. Historia inabainisha kuwa uhusiano huu ulianza katika Mkutano wa viongozi 29 wa kisiasa kutoka mataifa tofauti waliokutana katika mji wa Bandug, Indonesia mwaka 1955. Miongoni mwa watu mashuhuri walioshiriki mkutano huo ambao mwaka 2025 umetimiza miaka 70, ni aliekuwa Waziri Mkuu wa China, marehemu Zhou Enlai na aliekuwa kiongozi wa Chama cha TANU, marehemu Mwalimu Julius Nyerere. Mkutano wao hatimae ulizaa urafiki wa dhati na kidugu wa vyama vya siasa vilivyoshabihiana kiitikadi, TANU na Chama Cha Kikomunisti cha China (CPC), na baadae pamoja na ASP na hatimae CCM. Uhusiano huo umedumu na kutanuka na kuwa wa Kitaifa - Kidiplomasia, kiuchumi, mashirikiano ya watu na kistratejia.

Kwa mnasaba wa uhusiano huo wa kidugu, ni fahari na furaha kubwa kwangu kujumuika na viongozi na wanachama wa Chama kinachoongoza Tanzania, CCM, kuwakaribisha rasmi wasomaji katika toleo la kwanza la Jarida la Chama Cha Mapinduzi Tawi la China. Ni imani yangu kuwa maudhui yalio katika jarida hili yanayohusu CCM - historia na mwenendo wake, hali ya siasa, na ujenzi wa Taifa, yatafikisha taarifa na taswira sahihi kwa wasomaji wake ndani na nje ya China.

Inafurahisha kwamba Jarida hili linatolewa kwa lugha mbili ikiwemo Kiswahili. Lugha hii inatoa fursa sio tu ya kutanua hadhira ya kufikisha ujumbe wa maendeleo ya Tanzania na Chama Cha Mapinduzi nchini China, bali pia ya kukuza na kueneza lugha adhimu ya Kiswahili na utamaduni wa Tanzania.

Bila ya kupoteza madhumuni yake makuu, natumai kuwa Jarida hili litakuwa jukwaa la kutangaza fursa za uwekezaji – hususan katika viwanda vya kusarifu mazao kutoka sekta ya kilimo na madini. Jukwaa hili pia litatangaza vivutio vya kipekee vya utalii ilivyobarikiwa Tanzania ikiwemo mlima Kilimanjaro, maziwa ya Victoria, Tanganyika, Rukwa, Nyasa, na maeneo ya hifadhi na mbuga za wanyama kama Serengeti, Ngorongoro, Selous, na visiwa vya Zanzibar na Mafia. Historia, utamaduni, sanaa, fukwe, hali nzuri ya hewa na maeneo ya kimaumbile navyo ni vivutio vilivyotangazwa kwa wasomaji wa Jarida.

Kwa niaba ya Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini China, nawapongeza viongozi wa CCM – Tawi la China na wote waliowezesha maandalizi na kutolewa toleo hili la kwanza la jarida. Toleo la kwanza la jarida linaashiria safari ndefu ya Jarida iliopo siku za usoni. Viongozi, wahariri na wachapishaji wa Jarida wanapaswa kujizatiti ili kuhakikisha kuwa Jarida linakuwa endelevu lenye ubora unaotarajiwa, na likidhi kiu ya wasomaji.

## Kidumu Chama Cha Mapinduzi!



# Salamu za Katibu wa tawi la CCM China

Cde.
**Renatus Mahuyu**
*~Katibu wa Tawi la CCM China.*

## Ndugu Wanachama, Viongozi na Wapendwa Wasomaji,

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, kwa neema zake zisizokoma na kwa kutujaalia fursa hii ya pamoja. Kwa moyo mkunjufu na kwa heshima kubwa, nawakaribisha nyote katika jarida letu maalum la CCM Tawi la China – Toleo la Kwanza.

Jarida hili ni ushuhuda wa juhudi, weledi, na uzalendo wa wana CCM,wanaoishi mbali na nyumbani lakini wakiwa na Tanzania moyoni. Jarida hili ni kioo cha mchango wetu katika kujenga uchumi imara, elimu bora, na ushirikiano wa kimataifa wenye tija.

Katika jarida hili tumeonyesha ushirikiano wa muda mrefu kati ya China na Tanzania, ushirikiano ambao ni wa kihistoria, wenye mizizi yenye nguvu, na unaoendelea kuzaa matunda makubwa. Katika jarida hili, tumeonesha kwa undani jinsi ushirikiano huu umefungua milango ya ajira katika miradi ya kimkakati, fursa za uwekezaji kwa wajasiriamali wetu, na faida za kiuchumi zinazotia nguvu uchumi wa nchi yetu.

Pia. tumeelezea fursa za kielimu zinazopatikana kwenye nchi zote mbili na jinsi watanzania wanavyoweza kujiunga na vyuo vikuu bora vya China – vyuo vinavyoongoza duniani katika utafiti, uvumbuzi, na elimu yenye ubora wa hali ya juu. Tumeelezea pia michakato ya maombi, na hata ushirikiano wa serikali zetu mbili katika kutoa ufadhili. Hii ni ahadi yetu kwa kizazi kipya – Elimu ni haki, na jukumu la kuhakikisha kila Mtanzania anajua njia za kufikia ndoto zake ni letu sote.

Jarida hili pia limeelezea vivutio vya utalii vinavyopatikana Tanzania kuanzia urefu wa mlima Kilimanjaro hadi fukwe za kuvutia za Zanzibar, kutoka mbuga ya Serengeti hadi Selous na kuifanya nchi yetu kua ni tunu ya dunia. Kutangaza vivutio hivi kwa watanzania wazawa na wageni kutavutia watalii na wawekezaji kuja, kuona, na kushuhudia uzuri wa Tanzania.

Mwisho, tunatoa shukrani za pekee kwa wote waliofanikisha uwepo wa jarida hili – kutoka kwa wanachama wetu wa CCM tawi la China hadi kwa washirika wetu wa karibu na wadau mbalimbali. Karibuni tulisome na tujifunze zaidi kuhusu nchi yetu, chama chetu, kazi zetu, na mafanikio yetu. Tunathamini sana mrejesho wenu wenye tija ya kuboresha matoleo yajayo. Tuendeleeni kufanya kazi na kutumikia taifa letu kwa manufaa ya wote.

## Kidumu Chama Cha Mapinduzi!

"Uhusiano wa China na Tanzania ni Fursa ya kiuchumi kwa vijana wa Tanzania na jamii kwa ujumla" - Cde. Renatus Mahuyu



# Salamu za Shukrani kutoka kwa Mwenezi wa Tawi la CCM China

Cde.
## Mariam Ibrahim

*~Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi la CCM China.*

## Makomredi, Kidumu Chama Cha Mapinduzi.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya afya na uzima. Pili napenda kumpongeza na kumuombea heri, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania; Ndugu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza Chama kwa weledi mkubwa katika nyakati na vipindi vyote mpaka sasa. Kama Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, uongozi wake umebeba maono na dhamira ya dhati katika kuleta umoja, ushirikiano, amani ya kitaifa pamoja na maendeleo kwa Watanzania kupitia uwajibikaji madhubuti na uundwaji wa sera tofauti na makini kwa ajili ya maendeleo ya nchi, na Chama kwa ujumla.

Kwa nafasi tulio nayo kama vijana wa Chama Cha Mapinduzi nje ya Tanzania, tukiwa chini ya Tawi la Chama Cha Mapinduzi China, nipende kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Mwenyekiti wetu wa Tawi la CCM China; Cde. Hussein Ally Kanduru kwa kusimamia na kuongoza kamati iliofanikisha kukamilika kwa jarida hili. Haikua kazi nyepesi, bali yenye changamoto nyingi katika ukusanyaji, uhakiki na uhariri wa taarifa kwa vipindi tofauti ili kuhakikisha wasomaji wa jarida wanapata taarifa sahihi na zenye weledi.

Sanjali na shukrani hizi, nimshukuru pia Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara; Ndg. John Mongella kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha mchakato wa upatikanaji wa jarida hili. Pasipo kusahau, usimamizi na ushirikiano mkubwa tunao upata kutoka kwa kiongozi wetu, Mjumbe wa Kamati Kuu (MCC), na Katibu wa (NEC), Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Ndg. Rabia Abdalla Hamid kwa kutoa nafasi, na mazingira wezeshi yaliyo rafiki katika kukamilisha kazi ya jarida hili la Tawi la Chama Cha Mapinduzi China.

Wazo la kuwa na jarida la Tawi halikuanza kwenye uongozi huu, bali ni wazo lililoundwa na watangulizi wetu, hivyo napenda kutambua mchango wa Mwenyekiti wa Tawi la China kutoka mwaka 2022-2023, Cde. Given Ombeni Massawe, pamoja na uongozi wake wote ikijumuisha pia Mwenyekiti wa Tawi kutoka mwaka 2023-2024, Cde. Daudi Romani Manini na viongozi wote walio aminiwa kwa kipindi kilichopita kwa kuliendeleza wazo hili la kuwa na jarida na kuliweka katika utaratibu mzuri hatimae limekamilika na leo tumefanikiwa kupata jarida lenye taarifa zenye historia na kazi madhubuti zinazo simamiwa na Chama kupitia Tawi la China.

Aidha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Tawi, niwashukuru wote waliotoa muda pamoja na rasilimali zao katika kufanikisha kazi hii, ni ngumu kutaja kila mmoja wetu kwa nafasi zenu na kazi mliofanya, ila tambueni mchango wenu ni wa thamani kubwa katika Tawi la Chama Cha Mapinduzi China, na daima tutawakumbuka kupitia jarida hili.

Mwisho niwashukuru wanachama wote wa Tawi la CCM China kwa kuendeleza nidhamu njema kama makada watiifu na weledi hata nje ya mipaka ya Tanzania.

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Kidumu Chama Cha Mapinduzi.**



# WAANDAAJI WA JARIDA NA WAJUMBE WA KAMATI



## Cde. Hussein Ally Kanduru.
Mwenyekiti wa Kamati ya Jarida

email: kanduru007@gmail.com
Tell: +255 789 538 360.
Wechat ID: Kanduru007



## Cde. Isack Ibrahim Mrisho.
Katibu Kamati ya Jarida

Tell: +255 699 202 353



## Mwl. Yusuph Ally Rajab.
Itifaki na Maudhui



## Cde. Anthony Kassamali.
Mhariri wa Jarida

Tell: +1(564) 219-1984
email: info@nyaraka.com



## Abraham Issa Khalid.
Mbunifu wa Jarida

email: abrahamoik007@gmail.com
Tell: +255 620 773 449



## Cde. Munisi Sharon Emmanuel.

Mjumbe wa Kamati ya Jarida

email: sharonmunisi8@gmail.com
Tell: +1 (832) 903-0046
Wechat ID: Xuhanthedreamgal



## Cde. Renatus Mahuyu.


Mjumbe wa Kamati ya Jarida



## Cde. Janeth Nyandiwa Mnyaga.

Mjumbe wa na Kamati ya Jarida

Tell: +86 155 2780 7039



## Cde. Mphuru Neema Oberlin.

Mjumbe wa Kamati ya Jarida


email: mphuruneema@gmail.com



## Cde. Zaituni Abubakari.S.

Mjumbe wa Kamati ya Jarida

Tell: +255 656 634 075
email: smajamba@yahoo.com
Wechat ID: AbuuSasha



## Cde. Mariam Ibrahim.

Mjumbe wa Kamati ya Jarida



01

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

- *Historia ya Tawi la CCM China*
- *Viongozi wa Awali wa Tawi la CCM–China*
- *Muktadha wa Wanachama na Mfumo wa Uongozi*
- *Viongozi waliohudumu nafasi mbalimbali katika Tawi toka kuanzishwa kwake*
- *Walezi wa CCM China*
- *Viongozi wa Sasa wa Tawi la CCM China (2024/2025)*
- *Mashina ya Tawi la CCM China*

# UTANGULIZI

Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho tafsiri yake ya Kiingereza ni Revolutionary Party, ni chama tawala nchini Tanzania, na moja kati ya vyama vya siasa vilivyo kongwe na vyenye ushawishi mkubwa barani Afrika. Chama hiki kilianzishwa rasmi mnamo tarehe 5 Februari 1977, kutokana na muungano wa vyama viwili vya kisiasa vilivyokuwa na nguvu kwa wakati huo: TANU (Tanganyika African National Union) kutoka Tanzania Bara, na ASP (Afro-Shirazi Party) kutoka visiwani Zanzibar. Muungano huu uliunda chama kimoja imara, kilichopewa dhamana ya kuongoza katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

CCM ina matawi na mashina yaliyoenea kote nchini Tanzania. Aidha, Katiba ya chama inaruhusu kuanzishwa kwa matawi nje ya mipaka ya nchi, kama inavyo bainishwa katika Ibara ya 31, Kifungu cha 1(c). Matawi haya yanayo tambulika rasmi kama matawi ya CCM-Diaspora, na kwa msingi huo wa kikatiba, ndipo lilipoanzishwa rasmi Tawi la CCM-CHINA.

## Historia ya Tawi la CCM China

Kwa kuzingatia maono ya wanachama wa CCM waliokuwa wakiishi nchini China kwa zaidi ya miaka sita, ilidhihirika kuwa wengi wao waliendelea kuwa na imani na mapenzi ya dhati kwa Chama Cha Mapinduzi. Kutokana na hamasa hiyo, pamoja na juhudi za pamoja za waanzilishi, changamoto mbalimbali zilitatuliwa na hatimaye tawi la CCM-CHINA likaanzishwa mwishoni mwa mwaka 2014.

Wazo hili lilijikita katika msingi wa kikatiba kupitia Ibara ya 31(1)(c) ya Katiba ya CCM, inayoruhusu kuanzishwa kwa matawi ya chama nje ya nchi. Mchakato wa kuanzisha rasmi tawi ulianza tarehe 5 Februari 2014, na baada ya majadiliano ya kina pamoja na vikao vya maandalizi, Mkutano Mkuu wa Kwanza ulifanyika tarehe 4 Mei 2014, na viongozi wa mpito walichaguliwa rasmi, Cde. Boniphace S. Nobeji – Mwenyekiti; Cde. Olivo G. Mtunge – Katibu; Cde. Edgar T. Bebwa – Katibu wa Itikadi na Uenezi, na Cde. Joel Kayombo – Katibu wa Uchumi na Fedha

Kwa muktadha huo, barua rasmi ya kuomba utambuzi wa tawi iliandaliwa Oktoba 2014. Kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya mwaka 1997, sharti mojawapo ni kuwa na wanachama wasiopungua 70 ili tawi litambuliwe rasmi. Masharti hayo yalitimizwa, na hivyo Novemba 2014, Tawi la CCM–CHINA likapata utambulisho rasmi kutoka Makao Makuu ya CCM, chini ya idhini ya Katibu Mkuu wa Chama.

## Viongozi wa Awali wa Tawi la CCM–China

Baada ya kutambuliwa rasmi, viongozi wa kwanza wa tawi walikuwa ni Cde. Juma J. Mashenene – Mwenyekiti (Tianjin); Cde.Joel Kayombo – Katibu; Cde. Jafar R. Seifu – Katibu wa Itikadi na Uenezi (Wuhan); na Cde. Hilda L. Kaniki – Katibu wa Uchumi na Fedha.

## Muktadha wa Wanachama na Mfumo wa Uongozi

Tawi la CCM–CHINA linaundwa na wanachama wanaofanya shughuli mbalimbali, huku idadi kubwa wakiwa ni wanafunzi. Hali hii ilisababisha kuanzishwa kwa mfumo wa uongozi wa mwaka mmoja, ambapo kila mwanachama anayepewa dhamana ya uongozi hutumikia kuanzia mwezi Septemba hadi Julai ya mwaka unaofuata.

Mwaka 2015 ulifanyika uchaguzi mkuu wa kwanza wa tawi, na hapo ndipo uongozi wa mwaka 2015/2016 ulipoanza rasmi. Tangu wakati huo, mchakato huu wa kidemokrasia umeendelea kila mwaka bila kusitishwa hadi mwaka huu 2025, huku ukizingatia taratibu, maadili na misingi ya Katiba ya Chama Cha Mapinduzi.

## Viongozi waliohudumu nafasi mbalimbali katika Tawi toka kuanzishwa kwake

Ifuatayo ni orodha ya viongozi waliohudumu nafasi mbalimbali katika Tawi la CCM China toka Kuanzishwa kwake mwaka 2014. Mwaka 2014/2015 na 2015/2016 Cde. Joel kayombo na Cde. Hilda L. Kaniki walihudumu nafasi ya Katibu wa Uchumi na Fedha.

| MWAKA | MWENYEKITI | KATIBU | KATIBU WA ITIKADI NA UENEZI |
|---|---|---|---|
| 2014/2015 | Ndg. Dr Boniphase S Nobeji | Ndg. Olivo G Mtunge | Ndg. Edgar T Bebwa |
| 2015/2016 | Ndg. Juma J Mashenene | Ndg. Joel Kayombo | Ndg. Jafar R Seifu |
| 2016/2017 | Ndg. Tito Mateshi | Ndg. Juma Makaranga | Ndg. Otto John Matonya |
| 2017/2018 | Ndg. Michael Semindu | Ndg. Justina Joseph Mkumbi | Ndg. Marco Emmanuel Mwaimise |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | Ndg. Shauku Kihombo | Ndg. Nicas January Bernard | Ndg. Victoria Mwanziwa |
| 2019/2020 | Ndg. Salum Ramia | Ndg. Mabala Yazid | Ndg. Abdulwaheed Sarbouk |
| 2020/2021 | Ndg. Moses Werema | Ndg. Mahadhi Kisesa | Ndg. Muhsin Haji Ussi |
| 2021/2022 | Ndg. Muhsin Haji Ussi | Ndg. Given Ombeni Massawe | Ndg. Stephen Jeuma Bakari |
| 2022/2023 | Ndg. Given Ombeni Massawe | Ndg. Ghati Chacha Musabi | Ndg. Mahmoud Abdalla Mahmoud |
| 2023/2024 | Ndg. Daudi Romani Manini | Ndg. Amedeus Komu | Ndg. Feisal Suleiman |
| 2024/2025 | Ndg. Hussein Ally Kanduru | Ndg. Renatus Mahuyu | Ndg. Mariamu Ibrahim |



*Mwenyekiti wa kwanza wa tawi la CCM China Ndg. Dkt. Boniphase Nobeji (kushoto) akiwagawia kadi wanachama wa mwanzo wa Tawi la CCM China Kwenye moja ya vikao vya tawi mwaka 2014.*

# Walezi wa CCM China

Tawi la CCM China lina walezi kadhaa ambao wana dhamana juu ya maendeleo na ustawi wa Tawi, kushauri pale inapobidi kwa ajili ya ufanisi na utendaji wa Tawi letu. Ifuatayo ni orodha ya walezi wa Tawi la CCM China.

| NA. | JINA |
|---|---|
| 1 | Ndg. Khamis Mussa Omar |
| 2 | Ndg. Rabia Abdalla Hamid |
| 3 | Ndg. Dkt. Suleiman Serera |
| 4 | Ndg. Salim Ramia |
| 5 | Ndg. Remidius Mwema |
| 6 | Ndg. Asya Mwenda |
| 7 | Ndg. Ahidi J. Sinene |
| 8 | Ndg. Suleiman Mwenda |
| 9 | Ndg. Phelistas Wegesa |
| 10 | Ndg. Dkt. Benson Mugaka |
| 11 | Ndg. Mhandisi Yazid Mabala |
| 12 | Ndg. Kundo Mathew |
| 13 | Ndg. Victoria Mwanziva |
| 14 | Ndg. Michael Semindu |

# Viongozi wa Sasa wa Tawi la CCM China (2024/2025)

Ifuatayo ni orodha ya viongozi wanaohudumu katika nafasi mbalimbali za uongozi katika Tawi kwa mwaka 2024/2025.

| NA. | JINA | NAFASI |
|---|---|---|
| SEKRETARIETI YA TAWI | | |
| 1 | Ndg. Hussein Ally Kanduru | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Renatus Mahuyu | Katibu |
| 3 | Ndg. Mariamu Ibrahim | Katibu wa Itikadi na Uenezi |
| WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU | | |
| 1 | Ndg. Isack Ibrahim Mrisho | Mjumbe wa Kamati |
| 2 | Ndg. Juliana Gaithan Kauno | Mjumbe wa Kamati |
| 3 | Ndg. Leilat Ramadhan Aseid | Mjumbe wa Kamati |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Ndg. Martha Nehemia Mgalla | Mjumbe wa Kamati |
| 5 | Ndg. Peter Gottfried Msumali | Mjumbe wa Kamati |
| 6 | Ndg. Amani E Shayo | Mjumbe wa Kamati |
| 7 | Ndg. Sharon Emmanuel Munisi | Mjumbe wa Kamati |
| 8 | Ndg. Hamad Abdalla Ali | Mjumbe wa Kamati |
| 9 | Ndg. David Joseph Hassan | Mjumbe wa Kamati |
| 10 | Ndg. Mwalim Makame Mzee | Mjumbe wa Kamati |
| **WAJUMBE WA KAMATI YA SIASA** | | |
| 1 | Ndg. Hussein Ally Kanduru | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Renatus Mahuyu | Katibu |
| 3 | Ndg. Mariamu Ibrahim | Katibu wa Itikadi na Uenezi |
| 4 | Ndg. Martha Nehemia Mgalla | Mjumbe |
| 5 | Ndg. Hamad Abdalla Ali | Mjumbe |
| 6 | Ndg. David Joseph Hassan | Mjumbe |
| **KAMATI YA ELIMU NA MAFUNZO** | | |
| 1 | Mariamu Ibrahim | Mwenyekiti |
| 2 | Ramadhan Muharami | Katibu |
| **KAMATI YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)** | | |
| 1 | Ndg. Peter Gottfried Msumali | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Senzota Kivaria Semakua | Katibu |
| **KAMATI YA UCHUMI, MIPANGO NA FEDHA** | | |
| 1 | Ndg. Isack Ibrahim Mrisho | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Mwalim Makame Mzee | Katibu |

## *Mashina ya Tawi la CCM China*

Tawi la CCM China lina mashina katika miji tofauti ndani ya China yafuatayo ni mashina hai ya Tawi toka uongozi wa 2024/2025 kuingia madarakani. Hata hivyo uongozi wa Tawi kwa kushirikiana na wanachama wakereketwa wa Chama cha Mapinduzi katika miji mbalimbali wamefanikiwa kufufua baadhi ya mashina na kuongeza mashina mapya kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali.

| NA. | SHINA | MWENYEKITI | KATIBU |
|---|---|---|---|
| 1 | Beijing | Cde. Dkt. Joseph Kulwa Katobesi | Cde. Joseline Rajabu |
| 2 | Guangzhou | Cde. Ahmed Tamim | Cde. Sebastian Barenga |
| 3 | Wuhan | Cde. Dkt. Maimuna Abdi | Cde. Mahamudu J. Mnandeka |
| 4 | Shanghai | Cde. Juma Sima | Cde. Neema M. Angelile |
| 5 | Sichuan | Cde. Denis Chinamo | Cde. Fatma Omary Ally |
| 6 | Nanjing | Cde. Beatrice Nyallu | Cde. Beatrix Fedrick |
| 7 | Shandong | Cde. Tariq Abeid | Cde. Shafii Pella |
| 8 | Taiwan | Cde. Barnaba A. Buhombe | Cde. Leonard Y. Athumani |
| 9 | Hunan | Cde. Senzota K. Semakua | Cde. Jokha Mahmood |
| 10 | Zhejiang | Cde. Hemed Mbalu | Cde. Ikolewo E. Stanley |
| 11 | Jilin | Cde. Faruku M. Mpare | Cde. Juliana Kauno |
| 12 | Tianjin | Cde. Ramadhan Muharami | Cde. Othman Pascal Msalika |
| 13 | Xian | Sauli M. Kinahi | Seif Hamza Seif |

| NA. | SHINA | MWENYEKITI | KATIBU |
|---|---|---|---|
| MASHINA MAPYA | | | |
| 14 | Chongqing | Catherine Didas* | |
| 15 | Yunnan | Cde. Khalifa A. Omar* | Cde. Suleiman A. Mpechi* |
| 16 | Jinzhou | Cde. Somoe H. Farouk* | Cde. Lusako G. Mwakifwamba |
| 17 | Jiangxi | Ramlat A. haji* | |

* Viongozi wa muda kabla ya uchaguzi rasmi wa mashina mapya kufanyika



*Wenyeviti wastaafu wa Tawi la CCM China Cde. Given Ombeni Massawe (2022/23) wa kwanza kulia na Cde. Daudi Romani Manini(2023/24) wa pili kulia na Mwenyekiti wa Shina la Wuhan Cde. Dkt. Maimuna Iddy Abdi wa tatu kulia wakiwa katika picha ya pamoja na wanachama wa Shina la Wuhan baada ya kumalizika kwa kikao cha shina la Wuhan*

02

# SEHEMU YA PILI

## VIONGOZI WAKUU WA CHAMA CHA MAPINDUZI TOKA KUANZISHWA KWAKE

- *Wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tangu Kuanzishwa kwa CCM.*
- *Makamu Wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ZanzibarTangu Kuanzishwa kwa CCM.*
- *Makamu Wenyeviti wa CCM  Bara Tangu Kuanzishwa kwa CCM.*
- *Makatibu Wakuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tangu Kuanzishwa kwa CCM*
- *Nafasi za Manaibu Katibu wakuu wa CCM Zanzibar toka kuanzishwa kwa CCM*
- *Viongozi wa Idara za Chama cha mapinduzi (Wakuu wa Idara na Vitengo)*
- *Viongozi Wakuu wa Sasa wa Chama Cha Map-induzi (CCM)*
- *Jumuiya za Kitaifa za CCM (National Wings)*

# VIONGOZI WAKUU WA CHAMA CHA MAPINDUZI TOKA KUANZISHWA KWAKE

## A. Wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tangu Kuanzishwa kwa CCM.

Tangu kuasisiwa kwake, CCM imetoa dhamana kwa viongozi mahiri waliotoa mchango mkubwa katika kuimarisha dira na sera za chama, pamoja na mustakabali wa taifa kwa ujumla. Wenyeviti wa CCM waliowahi kushika hatamu za uongozi tangu mwaka 1977 katika vipindi tofauti:

| NA. | JINA | MUDA |
|---|---|---|
| 1 | Mwl. Julius Kambarage Nyerere | 1977-1990 |
| 2 | Ali Hassan Mwinyi | 1990-1996 |
| 3 | Benjamin William Mkapa | 1996-2006 |
| 4 | Jakaya Mrisho Kikwete | 2006-2016 |
| 5 | John Pombe Magufuli | 2016-2021 |
| 6 | Samia Suluhu Hassan | 2021- Mpaka sasa |

## B. Makamu Wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ZanzibarTangu Kuanzishwa kwa CCM.

| NA. | JINA | MUDA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Aboud Jumbe Mwinyi | 1977-1984 |
| 2 | Ndg. Ali Hassan Mwinyi | 1984-1990 |
| 3 | Ndg. Salmin Amour | 1990-2002 |
| 4 | Ndg. Amani Abeid Karume | 2002-2012 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Dkt. Ali Mohamed Shein | 2012-2022 |
| 6 | Dkt.Hussein Ali Mwinyi | 2022-Hadi sasa |

## C. Makamu Wenyeviti wa CCM Bara Tangu Kuanzishwa kwa CCM.

| NA. | JINA | MUDA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Aboud Jumbe Mwinyi | 1977-1984 |
| 2 | Ndg. Ali Hassan Mwinyi | 1984-1990 |
| 3 | Ndg. Rashid Mfaume Kawawa | 1990-1992 |
| 4 | Ndg. John Samwel Malecela | 1992-2012 |
| 5 | Ndg. Pius Msekwa | 2007-2012 |
| 6 | Ndg. Philip Japhet Mangula | 2012-2022 |
| 7 | Ndg. Abdulrahman Omary Kinana | 2022-2024 |
| 8 | Ndg. Stephen Masato Wasira | 2025-Mpaka sasa |



***Mwl. Julius Kambarage Nyerere***


***Aliekuwa Raisi wa Kwanza wa Tanzania na Mwenyekiti wa Kwanza wa Chama Cha Mapinduzi.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1977 hadi 1990***

***Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi***

***Aliekuwa Raisi wa Pili wa Zanzibar(1972-1984), Makamo wa Kwanza wa Raisi wa Tanzania(1972-1984), na Makamo Mwenyekiti wa Kwanza wa CCM Zanzibar.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1977 hadi 1984***



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi*

***Aliekuwa Raisi wa Pili wa Tanzania na Mwenyekiti wa Pili wa Chama Cha Mapinduzi.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1990 hadi 1996***

***Pia Alikua Makamo Mwenyekiti wa Pili wa CCM Zanzibar.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1984 hadi 1990***



***Mhe. Benjamin William Mkapa***


***Aliekuwa Raisi wa Tatu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tatu wa Chama Cha Mapinduzi.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1996 hadi 2006***

***Mhe. Salmin Amour***

***Aliekuwa Raisi wa Tano wa Zanzibar(1990-2000), Makamo wa Raisi wa Tatu wa Tanzania, na Makamo Mwenyekiti wa Tatu wa CCM Zanzibar***

***Uongozi wake ulianza mnamo 1990 hadi 2002.***



***Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete***

***Aliekuwa Raisi wa Nne wa Tanzania na Mwenyekiti wa Nne wa Chama Cha Mapnduzi.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 2006 hadi 2016***

***Mhe. Amani Abeid Karume***

***Aliekuwa Raisi wa Sita wa Zanzibar(2000-2010) na Makamo Mwenyekiti wa Nne wa CCM Zanzibar***

***Uongozi wake ulianza mnamo 2002 hadi 2012***



**Mhe. John Pombe Magufuli**

*Aliekuwa Raisi wa Tano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tano wa Chama Cha Mapinduzi.*

*Uongozi wake ulianza mnamo 2016 hadi 2021*

**Mhe. Ali Mohamed Shein**

*Aliekuwa Raisi wa Saba wa Zanzibar(2010-2020) na Makamo Mwenyekiti wa Tano wa CCM Zanzibar*

*Uongozi wake ulianza mnamo 2012 hadi 2022*



***Dkt. Samia Suluhu Hassan***

***Raisi wa Sita wa Tanzania na Mwenyekiti wa sita wa Chama Cha Mapinduzi.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 2021 mpaka sasa***

***Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi***

***Raisi wa Nane wa Zanzibar na Makamo Mwenyekiti wa Sita wa CCM.***

***Uongozi wake ulianza mnamo 2020 mpaka sasa***

# D. Makatibu Wakuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tangu Kuanzishwa kwa CCM

Katibu Mkuu wa CCM ni kiungo muhimu katika kusimamia shughuli za chama, kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya chama, na kuimarisha uhusiano kati ya chama na wanachama wake. Tangu kuanzishwa kwa CCM mwaka 1977, viongozi mbalimbali wamepata nafasi kwa vipindi tofauti kama ifuatavyo:

| NA. | JINA | MUDA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Pius Msekwa | 1977-1981 |
| 2 | Ndg. Daudi N Mwakawago | 1981-1982 |
| 3 | Ndg. Rashidi Mfaume kawawa | 1982-1990 |
| 4 | Ndg. Horace Kolimba | 1990-1995 |
| 5 | Ndg. Lawrence Gama | 1995-1997 |
| 6 | Ndg. Philip Mangula | 1997-2007 |
| 7 | Ndg. Yusuf Makamba | 2007-2011 |
| 8 | Ndg. Wilson Mukama | 2011-2012 |
| 9 | Ndg. Abdulrahman Kinana | 2012-2018 |
| 10 | Ndg. Bashiru Ally | 2018-2021 |
| 11 | Ndg. Daniel Chongolo | 2021-2023 |
| 12 | Ndg. Dkt. Emmanuel Nchimbi | 2024-2025 |
| 13 | Ndg. Dkt. Asha-Rose Migiro | 2025 hadi sasa |

# E. Nafasi za Manaibu Katibu wakuu wa CCM Zanzibar toka Kuanzishwa kwa CCM

| NA. | JINA | MUDA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Salmin Amour | 1977-1982 |
| 1 | Ndg. Allan Heri | 1979-1982 |
| 3 | Ndg. Ali Ameir Mohamed | 1990-1997 |
| 4 | Ndg. Hassan Musa Takrima | 1997-2000 |
| 5 | Ndg. Seif Ali Idd | 2000-2002 |
| 6 | Ndg. Salehe Ramadhani Ferouz | 2002-2011 |
| 7 | Ndg. Vuai Ali Vuai | 2011-2017 |
| 8 | Ndg. Abdullah Juma Saadaalla | 2017-2022 |
| 9 | Dkt. Muhammed Said Muhammed | 2022-Hadi sasa |

# F. Viongozi Wakuu wa Sasa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)

Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuongozwa na viongozi wanaolinda misingi yake, wakihimiza maendeleo ya siasa, uchumi na kijamii kwa manufaa ya Watanzania wote. Kwa sasa, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Ndg Samia Suluhu Hassan. Dkt. Samia ameandika historia kama mwanamke wa kwanza kushika nafasi hii ya juu kabisa katika chama na taifa, akiendelea kuongoza kwa busara, mshikamano na dira ya maendeleo jumuishi. Ifuatayo ni orodha ya viongozi wa juu kabisa wa chama Cha mapinduzi.

| NA. | JINA | NAFASI |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Dkt. Samia Suluhu Hassan | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Dkt. Hussein Ali Mwinyi | Makamo Mwenyekiti Zanzibar |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Ndg. Stephen Masato Wasira | Makamo Mwenyekiti Bara |
| 4 | Ndg. Dkt. Asha-Rose Migiro | Katibu Mkuu |
| 5 | Ndg. John Mongella | Naibu Katibu Mkuu Bara |
| 6 | Ndg. Mohammed Saidi Mohammed (Dimwa) | Naibu Katibu Mkuu Zanzibar |

## G. Viongozi wa Idara za Chama cha mapinduzi (Wakuu wa Idara na Vitengo)

Wafuataao wanashika nafasi katika Idara kuu za Chama Cha Mapinduzi

| NA. | JINA | NAFASI | IDARA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ndg. Issa Haji Ussi (Gavu) | Katibu wa NEC Organaizesheni | Organaizesheni |
| 2 | Ndg. Kenan Laban Kihongosi | Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo | Itikadi, Uenezi na Mafunzo |
| 3 | Ndg. Mirumbe Chacha | Katibu wa NEC of Uchumi na Fedha | Uchumi na Fedha |
| 4 | Ndg. Rabia Abdalla Hamid | Katibu wa NEC Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa | Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI) |

## H. Jumuiya za Kitaifa za CCM (National Wings)

Chama Cha Mapinduzi kina jumuiya tatu ambazo viongozi wake wanashika nafasi kama zinavyo onekana kwenye jedwali lifuatalo

| NA. | JINA | NAFASI |
|---|---|---|
| JUMUIYA YA WAZAZI | | |
| 1 | Ndg. Fadhili Maganya | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Dogo Iddi Mabrouk | Makamu Mwenyekiti |
| 3 | Ndg. Ally Salum Hapi | Katibu Mkuu |
| 4 | Ndg. Kirumbe Shaban Ng'enda | Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara |
| 5 | Ndg. Ali Issa Ali | Naibu Katibu Mkuu Zanzibar |
| UMOJA WA VIJANA WA CCM (UVCCM) | | |
| 1 | Ndg. Mohammed Ali Kawaida | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg.Rehema Sombi | Makamu Mwenyekiti |
| 3 | Ndg. Halid Mwinyi | Katibu Mkuu |
| 4 | Ndg. Mussa Peter Mwakitinya | Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara |
| 5 | Ndg. Abdi Mahmoud Abdi | Naibu Katibu Mkuu Zanzibar |
| UMOJA WA WANAWAKE WA TANZANIA (UWT) | | |
| 1 | Ndg. Mary Pius Chatanda | Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Zainabu Khamis Shomari | Makamu Mwenyekiti |
| 3 | Ndg. Suzan Peter Kunambi | Katibu Mkuu |
| 4 | Ndg. Riziki Mustafa Kingwande | Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara |
| 5 | Ndg. Tunu Juma Kondo | Naibu Katibu Mkuu Zanzibar |

# 03

# SEHEMU YA TATU

## UHUSIANO KATI YA TANZANIA NA CHINA: MTAZAMO WA KIHISTORIA

- *Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Tanzania na China – Reli ya TAZARA: Alama ya Ushirikiano Kati ya China na Tanzania.*
- *Mwendelezo wa Uhusiano*
- *Historia ya Tanzania chini ya TANU (Chama Cha Mapinduzi) na Harakati za Ukombozi Barani Afrika*
- *Ushawishi wa Tanzania*
- *Kambi Za Kijeshi Za Wapigania Uhuru Hapa Tanzania*
- *Uimarishaji wa siasa na namna Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Wanavyo Wasiliana na Wanachama Walioko China*

# UHUSIANO KATI YA TANZANIA NA CHINA: MTAZAMO WA KIHISTORIA

Uhusiano kati ya Tanzania na China ulianza mapema katika miaka ya 1960. Mara baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, ikifuatiwa na Zanzibar mwaka 1963. Tarehe 26 Aprili 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwelekeo wa kisiasa wa Tanzania awali ulikuwa na matokeo mbalimbali kutokana na misingi ya ujamaa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, iliyojikita katika kujitegemea, umiliki wa pamoja wa rasilimali, na msimamo thabiti dhidi ya ukoloni.

Wakati huo, China chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mao Zedong, ilijikita katika misingi ya ujamaa, kupinga ubeberu, na kutoshirikiana moja kwa moja na kambi yoyote ya kisiasa duniani. Misingi hii ya pamoja ya kiitikadi iliweka msingi wa ushirikiano wa kimkakati kati ya mataifa haya mawili.


China ilianza rasmi uhusiano wa kidiplomasia na Tanzania tarehe 26 Aprili 1964, hatua iliyoashiria mwanzo wa urafiki wa dhati na wa muda mrefu kati ya nchi hizi mbili. Rais Nyerere, katika ziara yake ya kwanza ya kiserikali nchini China, akitamka kua anatamani kila mtanzania angeweza kushuhudia kwa macho azma, mshikamano na mafanikio ya watu wa China.



***Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Mwenyekiti Mao Zedong (kulia) mwaka 1965***

Hata hivyo, Tanzania iliendelea kuunga mkono msimamo wa China katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa. Mnamo mwaka 1971, Tanzania ilikua miongoni mwa nchi zilizopiga kura kuunga mkono azimio la umoja wa Mataifa lililotambua Jamuhuri ya Watu wa China kama serikali halali ya nchi hiyo na kuiwezesha kuchukua kiti cha kudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Hatua hii iliimarisha nafasi na uhalali wa China katika mfumo wa kimataifa, huku ikiipatia Tanzania hadhi ya kisiasa na heshima kubwa katika ulingo wa diplomasia ya kimataifa kwa wakati huo.



*Balozi Dkt. Salim Ahmed Salim, mwanasiasa mahiri kutoka Tanzania, alitoa mchango mkubwa katika kutambuliwa kwa Jamhuri ya Watu wa China kama mwanachama halali wa Umoja wa Mataifa mwaka 1971, na kupokelewa rasmi ndani ya jumuiya hiyo ya kimataifa.*

## Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Tanzania na China – Reli ya TAZARA: Alama ya Ushirikiano Kati ya China na Tanzania.

Moja ya vielelezo muhimu vya ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na China ni Reli ya TAZARA. Hii ni miongoni mwa miradi ya awali inayoakisi uhusiano wa dhati kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China.

Reli hiyo ya mwaka 1970 hadi 1975, ikiwa na urefu wa maili 1,060 kutoka Dar es Salaam, Tanzania hadi Kapiri Mposhi, Zambia.Ujenzi wa reli hii ulifadhiliwa na Jamhuri ya Watu wa China kama mkopo wa muda mrefu usio na riba.

Mradi wa Reli ya TAZARA uliwapatia ajira maelfu ya Watanzania na uliunganisha maeneo mengi ya ndani ya nchi, hivyo kufungua fursa za kiuchumi na kuchochea maendeleo ya huduma katika maeneo mbalimbali.

Gharama za ujenzi wa reli hii zilifikia zaidi ya dola milioni 400 za Kimarekani, jambo linaloonesha dhamira ya kweli ya ushirikiano wa maendeleo kati ya mataifa haya mawili.



*Kituo cha mwisho cha reli ya TAZARA, Dar es Salaam, Tanzania (1976)*

## Mwendelezo wa Uhusiano

Uhusiano kati ya China na Tanzania umeendelea kuwa imara, ukiungwa mkono na misingi ya kiitikadi na historia ndefu ya ushirikiano wa kweli. Jiji la Dar es Salaam, Tanzania limekuwa makazi ya jamii kubwa ya Wachina, wakiwemo wahamiaji na wafanyabiashara.

Uwekezaji wa China nchini Tanzania, hususan katika sekta ya miundombinu, umechangia pakubwa kubadilisha sura ya uchumi wa taifa letu. Mataifa haya mawili yanaendelea kushirikiana kama wenza wa maendeleo, kwa msingi wa mshikamano, heshima, uaminifu, na dhamira ya pamoja ya kufanikisha malengo ya muda mrefu.



*Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa jamhuri ya watu wa China Xi Jinping*

# Historia ya Tanzania chini ya TANU (Chama Cha Mapinduzi) na Harakati za Ukombozi Barani Afrika

Katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika katika karne ya 20, Tanzania, chini ya uongozi wa chama cha TANU na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM), ilisimama kama mshirika wa kweli, mwaminifu na mwenye dhamira ya dhati katika vuguvugu la ukombozi barani Afrika.

Chini ya uongozi mahiri wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Tanzania iligeuka kuwa kimbilio salama kwa wapigania uhuru, ikiwezesha utoaji wa mafunzo ya kijeshi, msaada wa kidiplomasia, pamoja na vifaa vya kimkakati kwa mataifa yaliyokuwa yanapigania uhuru wao dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi.

Tanzania ilijikita kuwa kiungo muhimu na kinara, mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini, kwa kuruhusu Makao Makuu ya ANC kuendesha shughuli zake kutoka Tanzania. Kupitia umoja wa nchi huru za Afrika (OAU), Tanzania ilihimiza msimamo mkali dhidi ya ubaguzi wa rangi na kushinikiza jumuiya ya kimataifa kuwekea vikwazo vya kiuchumi na kisiasa Afrika Kusini hali ambayo iliongeza nguvu ya mapambano dhidi ya uvamizi wa Afrika Kusini.

Nchini Namibia, Tanzania iliunga mkono harakati za ukombozi wa SWAPO kuanzia mwaka 1960 hadi 1980, kwa kutoa mafunzo ya kijeshi, msaada wa kisiasa na mahusiano ya kidiplomasia, hatimaye kuchangia kupatikana kwa uhuru wa Namibia mwaka 1990.

Katika nchi ya Msumbiji, Tanzania ilitoa msaada mkubwa kwa chama cha FRELIMO kupambana na waasi waliokuwa wakisaidiwa na utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini. Tanzania ilichangia si tu kwa utaalamu wa kijeshi, bali pia kwa kuwa mwenyeji wa mazungumzo ya amani, hatua muhimu katika kufanikisha ukombozi wa taifa hilo.

Vivyo hivyo, harakati za ukombozi nchini Zimbabwe kupitia vyama vya ZANU na ZAPU zilipata hifadhi, msaada na usaidizi wa karibu kutoka Tanzania katika mapambano dhidi ya utawala wa kibaguzi wa Rhodesia. Kwa ujumla, Tanzania ilikuwa si tu nchi ya ukombozi, bali nguzo ya mshikamano barani Afrika, kusimamia haki, uhuru na utu wa Afrika.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Nelson Mandela*


## *Ushawishi wa Tanzania*

Ushawishi wa Tanzania ulizidi kuimarika, na kuifanya Tanzania kuwa msaada muhimu kwa serikali ya kijamaa ya Seychelles baada ya mapinduzi ya mwaka 1977. Hata hivyo, Tanzania ilichukua jukumu la kua mpatanishi mkuu katika mazungumzo ya amani mjini Arusha, kwa ajili ya kutafuta suluhu ya migogoro nchini Burundi na Rwanda.

Aidha, Tanzania iliisaidia kwa karibu Zambia katika mchakato wa kupata uhuru chini ya uongozi wa Kenneth Kaunda, na hata katika mataifa mengine kama Liberia, Komoro, na Guinea-Bissau, Tanzania ilisalia thabiti katika kutekeleza dhamira yake ya Upani-Afrika.

Kupitia vyama vya TANU na baadaye CCM, Tanzania haikutoa tu msaada wa kijeshi pekee, bali ilitumia pia ushawishi wake wa kidiplomasia kuendeleza ajenda za ukombozi wa Afrika.

Uaminifu wa Tanzania usiotetereka katika harakati za uhuru, haki na utu duniani, ulichangia kwa kiasi kikubwa katika kuikomboa Afrika kutoka katika minyororo ya ukoloni. Hatua hizi ziliifanya Tanzania kuwa nguzo ya mshikamano barani Afrika urithi wa kudumu wa utu, mshikamano na matumaini.



*Samora Machel na Julius Kambarage Nyerere wakiwa Dar es Salaam (1978)*



*Kuunga Mkono Mapambano Dhidi ya Ubaguzi wa Rangi na Ukoloni*




*Wanajeshi wa Tanzania nchini Seychelles (miaka ya 1970)*

# Kambi Za Kijeshi Za Wapigania Uhuru Hapa Tanzania

Katika kipindi cha harakati za ukombozi barani Afrika, Tanzania ilitoa maeneo maalum kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika. Kwa moyo wa mshikamano wa kweli na dhamira isiyoyumba ya kulikomboa Bara la Afrika dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi, nchi yetu iliwahifadhi, kuwalea na kuwaandaa wapiganaji kwa ajili ya mapambano ya ukombozi wa mataifa yao.

Baadhi ya maeneo mashuhuri yaliyokuwa kambi za mafunzo ya kijeshi yameainishwa katika ramani hapa chini:




*Kambi tofauti za wapigania uhuru nchini Tanzania*

# Uimarishaji wa siasa na namna Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Wanavyo Wasiliana na Wanachama Walioko China

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na mataifa yenye historia ya ushirikiano wa karibu na Tanzania. Miongoni mwa mataifa hayo, Jamhuri ya Watu wa China inashikilia nafasi ya kipekee kama mshirika wa karibu wa Tanzania tangu enzi za baada ya uhuru.

Katika kuendeleza mshikamano huu wa kihistoria, CCM huandaa ziara rasmi nchini China zenye lengo la kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia, kutoa mafunzo ya kisiasa, na kujenga uwezo kwa makada wa chama. Ziara hizi ni nguzo muhimu katika kuimarisha itikadi ya chama, kuendeleza mahusiano ya kimataifa, na kubadilishana uzoefu katika maeneo ya utawala bora, uchumi, na maendeleo endelevu.

Moja ya vipengele muhimu katika ziara hizi ni mashauriano ya moja kwa moja kati ya wajumbe kutoka Tanzania na wanachama wa CCM walioko China—wakiwemo wanafunzi, wafanyabiashara, wataalamu na wafuasi wa chama. Kupitia mijadala na mikutano ya kimkakati, chama huhakikisha kuwa wanachama wake walioko nje ya nchi wanaendeleza dira, misingi na sera za chama kwa uaminifu.

Katika miaka ya hivi karibuni, mikutano hii imepata uzito mkubwa, ikihudhuriwa na viongozi wa ngazi ya juu kutoka serikalini na ndani ya chama, wakiwemo wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Hii imekuwa sehemu muhimu ya kudumisha mshikamano wa kiitikadi, kukuza mijadala ya maendeleo, na kuhamasisha Watanzania wanaoishi China kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa lao.

Katika mazingira ya kuimarisha falsafa ya uongozi, mahusiano haya yanathibitisha dhamira ya kweli ya CCM katika kujenga mshikamano wa kimataifa, huku ikihakikisha kuwa Watanzania walioko nje ya nchi wanabaki kuwa sehemu hai ya mchakato wa kisiasa na maendeleo ya taifa.

Mahusiano endelevu kati ya CCM na wanachama wake walioko China ni kielelezo halisi cha ushirikiano wa kimkakati unaozidi kuimarika na kuimarisha umoja wa kitaifa katika ngazi ya kimataifa.




*Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi Tawi la China siku ya Tarehe 3/6/2025 walimpokea mlezi wa Tawi ambae ni Mjumbe wa Kamati kuu (MCC) na Katibu wa (NEC) mambo ya siasa na Uhusiano wa Kimataifa Ndg. Rabia Abdalla Hamid pamoja na ujumbe wake walipotembelea China kwa ziara maalum ya kikazi.*





***Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar***

*Dkt. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akiwa pamoja na Balozi wa Tanzania nchini China, Khamis Mussa Omar (kulia), katika picha ya pamoja na baadhi ya wanachama wa tawi la CCM China mjini Sanghai.*




***Aliekua Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)***

*Ndugu Emmanuel John Nchimbi na Makamu wa Raisi wa Tanzania (katikati), akiwa pamoja na wanachama wa Shina la CCM mjini Beijing.*



### Aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM,

*Ndg. Daniel Godfrey Chongolo, pamoja na Balozi wa Tanzania nchini China kati ya mwaka 2017 hadi 2023, Ndg. Mbelwa Kairuki (katikati), pamoja na wajumbe wa Kamati Kuu na wanachama wa Shina la CCM mjini Guangzhou.*



### Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara

*Ndugu John Mongella(wa pili kushoto), Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, Ndugu Ally Hapi (wa pili kulia), Mbunge wa Jimbo la Malindi MNEC Muhsin Ussi(Kushoto), Mwenyekiti wa Shina la Beijing, Ndugu Joseph Katobesi(Kulia) Kwenye picha pamoja na wanachama wa Shina la Beijing.*



***Makamo Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi***

*Ndg. John Mongella (wa pili kulia) akiwa pamoja na viongozi wa waandamizi wa Tawi la CCM China pamoja na Shina la Hunan Ndg. Senzota Kivaria Semakua (Kushoto), Ndg. Daudi Roman Manini (wa pili kushoto) na Ndg. Hussein Ally Kanduru (Kulia) alipowatembelea viongozi wa Shina hilo mji wa Changsha, Hunan.*




***Mjumbe wa Kamati Kuu (MCC) na Katibu wa (NEC), mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI)***

*Ndg. Rabia Abdalla Hamid (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na uongozi wa Tawi la Chama Cha Mapinduzi (CCM) China, likiongozwa na Mwenyekiti wake Ndg. Hussein Ally Kanduru (wa nne kushoto) pamoja na Katibu wa Siasa na Uenezi (M) Songwe, Ndg. Yusuph Ally Rajabu (wa kwanza Kulia), kwenye ziara yenye lengo la kuimarisha mshikamano wa wanachama wa CCM walioko nje ya nchi.*




***Baadhi ya wanachama wa Tawi la CCM China***

*waliojitokeza Juni 2025 kumpokea Mjumbe wa kamati Kuu (MCC) na Katibu wa (NEC), mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Ndg. Rabia Abdalla Hamid, alipotembelea mji wa Beijing, China kwa ziara maalum ya kichama tarehe 3/6/2025.*




***Mjumbe wa Kamati Kuu (MCC) na Katibu wa (NEC) mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa***

*Ndg. Rabia Abdalla Hamid akifanya kikao na wanachama wa Tawi la CCM China kilichofanyika mjini Beijing siku ya Tarehe 4/6/2025.*



# 04 SEHEMU YA NNE

## CCM NA AJENDA ZA MAENDELEO:

### Mafanikio ya Ilani ya CCM ya 2020–2025

1. Sekta ya Uchumi
2. Sekta ya Afya
3. Sekta ya Elimu

### Dondoo za ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu kwa mwaka 2025 - 2030

## CCM NA AJENDA ZA MAENDELEO:

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeendelea kuwa na ushawishi mkubwa ndani ya Tanzania na barani Afrika kwa ujumla, kutokana na utekelezaji thabiti wa ilani zake za uchaguzi ambazo zimechangia pakubwa katika kuleta miradi ya maendeleo yenye mageuzi ya kweli. Katika kipindi cha miaka mitano (2020 – 2025), chama kimefanikiwa kukamilisha na kuanzisha miradi yenye tija kwa jamii ya Watanzania.

Katika kipindi hicho, Serikali ya awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetekeleza kwa mafanikio makubwa falsafa ya "4R" inayojumuisha: Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi, na Ujenzi Upya. Falsafa hii imeimarisha demokrasia ya vyama vingi, kudumisha utulivu wa kisiasa, na kuendeleza amani na umoja wa kitaifa misingi muhimu ya maendeleo ya kijamii na uchumi. Katika kipindi chote cha utekelezaji, falsafa ya 4R imekuwa nguzo muhimu ya maendeleo endelevu na demokrasia jumuishi ya Tanzania.

# *Mafanikio ya Ilani ya CCM ya 2020–2025*

Kupitia Serikali ya Awamu ya Sita, CCM imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani yake ya mwaka 2020-2025. Mafanikio haya yameonekana katika nyanja mbalimbali, ikiwemo uchumi, jamii na siasa. Serikali imechukua hatua madhubuti za kuimarisha huduma muhimu za kijamii kama vile afya, elimu, na maji kama ifuatavyo:

## 1. SEKTA YA UCHUMI

### i) Ukuaji wa pato la Taifa

KUTOKA: *4.8%, MWAKA 2020* → MPAKA: *4.8%, MWAKA 2020*

### ii) Ongezeko la mapato ya kodi

KUTOKA: *Tril 20.59/=, MWAKA 2020/21* → MPAKA: *Tril 20.59/=, MWAKA 2020/21*

### ii) Ongezeko la ajirakupitia miradi mikubwa kama vile, bomba la mafuta ghafi la Africa la mashariki, ujenzi wa leri ya kisasa ya SGR na ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la mwalimu nyerere.

AJIRA MPYA: **8,084,204**

# 1. SEKTA YA AFYA

## i) Ongezeko la bajeti ya Afya kwa 32.29%

KUTOKA: *Bilioni 1.92 mwaka 2020/21* → MPAKA: *Trilioni 2.54 mwaka 2024/25*

## ii) Ongezeko la vituo 4063 vya kutoa huduma za Afya


KUTOKA: *8783, mwaka 2020* → MPAKA: *12,846, mwaka 2025*

## iii). Kutungwa kwa sheria ya bima ya afya kwa wote ya mwaka 2023 ili kuandaa utaratibu wa kugharamia huduma za afya kwa wananchi.

# 1. SEKTA YA ELIMU


### i).Elimu bila ada

Kuendelea kutekelza mpango wa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi hadi kidato cha sita kwa kuongeza fedha za kugharamia mpango huo kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020 hadi hadi shilingi bilioni 484.27 mwaka 2025 na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mpango huu kuzidi wanafunzi milioni mbili.





### ii).Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya vyuo vya kati wanaosoma stashahada ya fani ya ufundi hadi kufikia wanafunzi 7534.




### iii).Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu

Kuongezeka kwa bajet ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 787.4 mwaka 2025



# Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya uchaguzi mkuu kwa mwaka 2025 - 2030

Lengo kuu la Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2025-2030 ni kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi. Ilani hii ni nyenzo ya CCM katika kuanza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2025 - 2030 imejikita katika vipaumbele nane vifuatavyo:

## MAPINDUZI YA UCHUMI WA KISASA

*i). Kuchochea mapinduzi ya uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasilimali zinazozalishwa nchini;*



## FURSA ZA AJIRA KWA VIJANA

*ii). Kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini;*



## MAISHA BORA KWA WOTE

*iii). Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii;*



## MABORESHO KATIKA SEKTA YA USAFIRI

*iv). Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji;*



## TEKNOLOJIA KWA MAENDELEO

*v). Kukuza na kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumi na kijamii;*



## DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA

*vi). Kudumisha demokrasia na utawala bora;*



## AMANI, UTULIVU NA USALAMA.


*vii). Kuendelea kudumisha amani, utulivu na usalama;*

**NGUZO ZA TAIFA BORA**



## TAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*viii). Kudumisha utamaduni wa taifa, na kukuza sanaa na michezo.*



Kwa kuzingatia lengo na vipaumbele hivyo, Chama Cha Mapinduzi kinawaomba wananchi wote wa Tanzania kuendelea kukiunga mkono kwa kuwachagua kwa kura nyingi za NDIYO wagombea wake wote wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Dkt. Samia Suluhu Hassan na Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi nafasi ya Makamo wa Raisi, Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kumpigia kura nyingi za NDIO Dkt. Hussein Mwinyi, Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi watakaopitishwa na vikao halali vya Chama, na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

CCM inawaahidi Watanzania wote kuwa itaendelea kuisimamia Serikali kutekeleza kikamilifu ahadi na maelekezo yaliyotolewa katika Ilani hii ili kufikia malengo yaliyowekwa. Aidha, CCM itahakikisha kuwa, katika utekelezaji wa Ilani hii, Serikali na vyombo vyake vyote inazingatia weledi, haki, na usawa, na kwamba rushwa na ubaguzi wa aina zote vinapigwa vita kama maadui wakubwa wa maendeleo ya jamii na Taifa.

05

# SEHEMU YA TANO

## *VIVUTIO VYA UTALII NCHINI TANZANIA*

- *Kanda ya kaskazini - Moyo wa Utalii wa Wanyamapori Tanzania.*
- *Kanda ya Kusini: Uzuri wa Asili Usio na Mchafuko*
- *Kanda ya Magharibi: Moyo wa Pori wa Tan-zania*
- *Kanda ya Mashariki: Mahali Ambapo Bio-anuai Hukutana na Uzuri wa Pwani*
- *Vivutio Vya Utalii Visiwani Zanzibar*

## VIVUTIO VYA UTALII NCHINI TANZANIA

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa vivutio vya utalii barani Afrika, ikiwa imebarikiwa na mandhari ya kipekee, wanyamapori wa aina mbalimbali, na urithi wa kitamaduni usio na kifani. Ikiwa na mbuga 22 za taifa pamoja na hifadhi nyingine nyingi za wanyamapori, Tanzania inatoa kumbukumbu nzuri na kipekee Katika safari za kitalii ambayo ni nadra kupatikana mahali pengine duniani.

Miongoni mwa Mbuga maarufu za utalii nchini Tanzania ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, inayotambulika kimataifa kwa uhamaji mkubwa wa nyumbu, pamoja na Kreta ya Ngorongoro, eneo la urithi wa dunia linalovutia maelfu ya watalii kila mwaka kutokana na mandhari yake ya kipekee na historia ya kiutamaduni.

Aidha, Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo ya pori ambayo yasiyo fahamika, lakini yanabeba uzuri wa kipekee wa asili, kama vile hifadhi ya Taifa ya Nyerere (iliyokuwa Selous) na hifadhi ya Ruaha. Maeneo haya huvutia zaidi watalii wanaopenda ukimya wa mazingira ya asili usioingiliwa na shughuli nyingi za binadamu.

Maeneo haya yaliyohifadhiwa kwa umakini mkubwa ni makazi ya wanyama watano wakubwa (The Big Five) Simba, Tembo, Nyati, Chui, na Kifaru ikihusisha ndege, mimea nadra, na mandhari ya kuvutia. Uzuri huu wa kipekee umeifanya Tanzania kuwa chaguo mashuhuri kwa watalii kutoka duniani kote.



Mbuga za taifa zinachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa taifa na kuiimarisha taswira ya nchi kimataifa. Hifadhi hizi huwapokea mamilioni ya wageni kila mwaka, na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii, sambamba na kuonesha dhamira ya dhati ya Tanzania katika uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.

Kwa lengo la kuonesha na kulinda urithi wake wa kibayolojia, maeneo ya hifadhi nchini yamegawanywa katika kanda kuu nne, kila moja ikiwa na mifumo ya kiikolojia ya kipekee, inayohifadhi urithi wa asili na kuwanufaisha wananchi wa maeneo husika kijamii na kiuchumi.

# *Kanda ya kaskazini - Moyo wa Utalii wa Wanyamapori Tanzania.*

Kanda ya Kaskazini ndiyo kitovu maarufu zaidi cha utalii nchini Tanzania. Eneo hili huvutia wageni kutokana na uwanda wake mpana, mandhari ya kupendeza, na bioanuwai isiyo na kifani. Ndani ya kanda hii kunapatikana tukio la kihistoria la uhamaji mkuu wa wanyama (Great Migration); Kaldera ya Ngorongoro ni moja ya mandhari ya kuvutia zaidi duniani; na Mlima Kilimanjaro - mlima mrefu zaidi barani Afrika. Kanda hii si tu msingi wa sekta ya utalii nchini, bali pia ni alama ya fahari ya taifa kwa uzuri wake wa asili unaotambulika kimataifa.

## *Hifadhi ya Taifa ya Serengeti*

Serengeti ni moja wapo ya hifadhi pendwa na maarufu zaidi barani Afrika ni sehemu ya Urithi wa dunia wa UNESCO. Inatambulika duniani kote kwa tukio la kipekee la Uhamaji Mkuu wa Wanyama, ambapo zaidi ya nyumbu milioni 1.3, pundamilia, na wanyamapori wengine husafiri kwa makundi makubwa, wakihama kutoka eneo moja hadi jingine wakitafuta malisho na maji safi. Uhamaji huu wa kuvutia hutokea kati ya Aprili hadi Julai, wanyama huvuka maeneo makubwa ya savana, na kuvutia maelfu ya wageni kutoka kila pembe ya dunia kushuhudia maisha ya wanyama wanaowinda na wanaowindwa kwa karibu.



Kwa jina la asili la “Siringet” kwa Kimasai, likiwa na maana “uwanda usio na mwisho”, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni alama ya fahari ya Tanzania. Iko katika Kanda ya Kaskazini, hifadhi hii ni moja ya maeneo ya kipekee duniani yenye mfumo hai wa ikolojia, unaohifadhi mamia ya aina za wanyamapori.

Miongoni mwa wanyama wanaopatikana hapa ni simba, duma, fisi, swala, pofu wa Cape, nyumbu, na pundamilia, ambao huishi katika mazingira ya savana yenye uwanda mpana na vilima vinavyojipinda kwa haiba ya kipekee.

Mandhari ya kuvutia ya Serengeti huvutia wapenda mazingira, wapiga picha wa kitaalamu, kutoka kote duniani wakitafuta na kushuhudia uzuri wa asili katika hali yake halisi, isiyoingiliwa na mikono ya binadamu.

Serengeti pia ni hifadhi ya maisha (Biosphere Reserve) inayotambuliwa na UNESCO, ikijivunia bioanuwai ya kipekee inayojumuisha mamia ya spishi za ndege na wanyamapori, kuanzia simba wanaowinda kwa ustadi, hadi duma wanaokimbia kwa kasi, kila kona ya Serengeti hutoa taswira halisi ya pori la Afrika pori lililojaa uzuri wa asili usioguswa, unaovutia na kugusa hisia za kila mgeni anayepata nafasi ya kulitazama.

Zaidi ya kuwa kivutio cha kipekee cha utalii, Serengeti ni mfano halisi wa dhamira ya Tanzania katika kulinda mazingira na urithi wake wa asili.

Hii si tu hifadhi ya taifa, bali ni ushuhuda hai wa kujitolea kwa taifa katika kuhifadhi na kuendeleza hazina ya vizazi vyetu, urithi usioguswa na wakati.

Kwa yeyote anayetafuta safari isiyosahaulika, na inayogusa moyo, Serengeti ni mlango wa kuingia katika moyo wa Afrika ya porini safari ya asili isiyo na mipaka.







## *Eneo la Hifadhi la Ngorongoro*

Ngorongoro ni mbuga yenye maajabu ya kipekee duniani, ikijivunia kuwa na kaldera kubwa zaidi isiyo na shughuli za volkano na iliyohifadhiwa kikamilifu.

Eneo hili si tu hifadhi ya wanyamapori, bali ni mandhari ya kuvutia, kijiolojia na yenye historia ya kipekee, sambamba na kuwa makazi ya jamii ya Wamasai, jambo linaloongeza uzito wa mvuto wa kiutamaduni na urithi wa kihistoria unaovutia wageni kutoka pande zote za dunia.

Ngorongoro ni hifadhi maarufu inayo patikana kaskazini mwa Tanzania, ni sehemu ya urithi wa dunia inayodhihirisha uzuri wa kipekee wa nchi yetu. Katika savana zake pana, hupatikana wanyama mashuhuri kama simba, tembo, kifaru, nyati, na chui—wanaojulikana kama “The Big Five.”


Mandhari yake maridadi huvutia maelfu ya watalii kutoka kila kona ya dunia, huku maisha ya wanyamapori yakichanganyika na maisha ya binadamu, hasa jamii ya Wamasai, wanaoishi ndani ya hifadhi kwa utulivu na ushirikiano wa asili.

Kwa yeyote anayetaka kugusa moyo wa urithi wa Tanzania, Ngorongoro ni hifadhi muhimu kwa utalii wa ndani











## *Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro*

Mlima Kilimanjaro, mlima mrefu zaidi barani Afrika na volkano huru ndefu zaidi duniani, ni mojawapo ya maajabu ya kiasili yanayovutia maelfu ya wageni kutoka kila pembe ya dunia.


Kupanda mlima kilimanjaro hakutoi tu changamoto ya kimwili pekee kwa mpandaji, bali pia ni safari ya kiroho na ushindi inayowazawadia wanao thubutu safari hii, mandhari ya kipekee itakayoacha kumbukumbu nzuri isiyosahaulika mara baada ya mpandaji kufika kwenye kilele cha mlima huu.

Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, inayopatikana kaskazini mwa Tanzania, ni kilele maarufu cha Kibo (mita 5,895) chenye barafu za kudumu, pamoja na vilele vingine, Mawenzi (mita 5,149), na Shira (mita 3,962).

Hifadhi hii ina mandhari ya kuvutia, kuanzia misitu yenye uoto mnene hadi jangwa la alpine katika maeneo ya juu, na inajumuisha mfumo wa ikolojia unaobadilika kwa hatua kadri unavyopanda mlima Kilimanjaro

Kiwango cha mvua katika mlima huu hubadilika kulingana na mwinuko: kutoka milimita 828 katika maeneo ya juu, hadi zaidi ya milimita 2,500 kwenye misitu ya milimani ikiashiria utajiri mkubwa wa kijiografia na kiikolojia wa eneo hili la urithi wa dunia.





*Kilele cha Mlima Kibo (Mlima Kilimanjaro)*



*Kilele cha Mlima Mawenzi*

Watalii wa hifadhi ya Kilimanjaro hupata fursa ya kipekee ya kushuhudia uzuri wa misitu ya kitropiki, mandhari ya milima yenye ukimya, na hatimaye, barafu za Kibo juu ya paa la Afrika. Ni kivutio kisicho na mfano kwa wapenda mazingira, wapandaji wa milima, na wasafiri wanaotafuta uzoefu wa kipekee.

Kilimanjaro si tu alama ya kijiografia, bali ni nembo ya fahari ya taifa la Tanzania. Ni sehemu ya urithi wa dunia unaothibitisha uzuri wa mazingira yetu ya asili na dhamira ya kulinda rasilimali hizi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## *Hifadhi ya Taifa ya Arusha*

Inapatikana karibu na mji wa Arusha, Hifadhi ya Taifa ya Arusha yenye mandhari ya kuvutia na misitu ya mvua, tambareare za wazi, na Mlima Meru unaosimama kwa upekee wa kuvutia

Hifadhi hii ni mahali bora kwa Safari za magari (game drives); Matembezi ya miguu (walking safaris); Uchunguzi wa ndege (birdwatching). Ni chaguo mahsusi kwa wageni wanaopenda uhusiano wa karibu na mazingira ya asili, wakitafuta utulivu, mafunzo, na uzuri wa kimyakimya wa porini.

Kanda ya Kaskazini imeendelea kuwa kitovu cha utalii nchini Tanzania, ikiwavutia mabalozi, watafiti, na watalii wa kimataifa wanaojali masuala ya uhifadhi wa mazingira na urithi wa asili.

Kupitia vivutio vyake vya kipekee na bioanuwai isiyo na mfano, Tanzania imejidhihirisha kuwa chaguo kuu barani Afrika kwa wapenda mazingira na wale wanaotafuta safari za kusisimua zenye maana ya ndani, utulivu wa kiroho, na mafunzo ya maisha ya asili.



*Kilele cha Mlima Meru katika Hifadhi ya Arusha*

## Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

Hifadhi ya Taifa ya Tarangire inatambulika kwa makundi makubwa ya tembo na mifumo mbalimbali ya ikolojia inayovutia. Hifadhi hii hutoa uzoefu halisi wa safari za mwituni, kupitia mandhari yanayojumuisha misitu ya asili, maeneo ya maji ya msimu, na savana za wazi zinazowapa wageni hisia ya kuungana na mazingira ya porini kwa namna ya kipekee.



## Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara

Ziwa Manyara ni hifadhi tulivu iliyoko katika bonde la ufa, inayojulikana kwa wingi wa ndege, hususan korongo (flamingo), pamoja na mandhari ya kijani yenye utulivu wa kipekee.

Ni eneo mapumziko ya kipekee kwa wapenda utalii wa kimya, utulivu na mandhari halisi ya asili. Kwa wale wanaotafuta safari ya utulivu wa ndani, Ziwa Manyara huwapa ukaribu na maisha ya porini katika hali ya amani isiyo na msongamano.



# Kanda ya Kusini: Uzuri wa Asili Usio na Mchafuko

Kanda ya Kusini ya Tanzania ni hazina ya safari tulivu na ya kipekee, mbali na mikondo ya utalii wa halaiki. Eneo hili limejaa savana pana, misitu minene, na kingo za mito zenye uhai, likiwa kimbilio kwa wapenda mazingira na watafiti wa uhifadhi wanaotafuta sura halisi ya pori la Afrika.

Hifadhi na mapori ya akiba ya Kanda hii yanatambulika kwa utulivu wake, aina nyingi za wanyamapori, na mandhari safi ya kuvutia macho na kugusa moyo. Kwa yeyote anayetamani safari ya kina, yenye mawasiliano ya karibu na mazingira ya asili, Kanda ya Kusini ni chaguo linalotoa utulivu wa kweli na uzuri usioguswa wa Tanzania.

## Hifadhi ya Taifa ya Ruaha:

Ikiwa na zaidi ya kilomita za mraba 20,000, Ruaha ni hifadhi ya pili kwa ukubwa nchini Tanzania na moja ya maeneo muhimu zaidi ya bioanuwai barani Afrika. Ni nyumbani kwa viumbe adimu kama kudu mkubwa na paa wa sable, wanaopatikana kwa nadra katika maeneo mengine ya bara hili.


Nyanda zake za majani ni zenye upana na kingo za mito zenye kuvutia, makundi makubwa ya tembo, simba, na wanyama wengine wanaowinda, na kuifanya Ruaha kuwa mahali bora kwa uchunguzi wa maisha ya porini katika hali yake halisi. Kwa wapenda mazingira wanaotafuta uzuri wa kipekee, Hifadhi ya Ruaha hutoa uzoefu wa safari isiosahaulika, mahali ambapo sauti ya pori bado inasikika kwa uwazi na utulivu.



## *Hifadhi ya Taifa ya Katavi: Pori Takatifu la Mwisho wa Dunia*

Katavi ni moja ya hifadhi za kipekee zinazopatikana katika maeneo ya mbali kabisa ya Tanzania, na ndiyo maana uzuri wake wa asili umehifadhiwa kwa umakini. Ni mbuga isiyoguswa na maendeleo ya kisasa, inayowapa wageni fursa ya pekee.

Katika nyanda hii tulivu, makundi makubwa ya nyati, tembo, na aina nyingi za ndege huishi kwa uhuru, wakichanganyika na mandhari ya asili. Kwa wasafiri wanaotafuta safari ya kweli yenye utulivu wa kina na pekee, Katavi ni hazina iliyojificha, mahali ambapo utulivu na uzuri wa Tanzania ya asili unaendelea kung’aa bila bugudha.



*Twiga katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi*

## *Hifadhi ya Taifa ya Kitulo: Serengeti ya Maua*

Kitulo, inayojulikana kwa jina la kuvutia la "Serengeti ya Maua," ni hifadhi ya kipekee ya nyanda za juu inayojivunia mashamba ya maua pori yenye rangi angavu, hasa katika msimu wa maua ya aina ya orchid.

Ni mahali pa ndoto kwa: Wataalamu wa mimea; Wapiga picha wa mandhari; Wapenzi wa maumbile wanaothamini uzuri wa utulivu na asili ya kweli;.

Kitulo iko katika nyanda za juu za Kanda ya Kusini, Kitulo huwasilisha sura tofauti ya Tanzania—iliyotulia, isiyoguswa, na ya kuvutia kwa namna yake ya kipekee. Kwa wasafiri wanaotafuta utulivu wa ndani, mbali na mikondo ya kawaida ya watalii, Kitulo ni mwaliko wa safari ya kina, inayosimulia uzuri wa Tanzania katika umbo lake halisi na lisiloguswa.



# Kanda ya Magharibi: Moyo wa Pori wa Tanzania

Kanda ya Magharibi ni ardhi yenye uzuri wa asili usioguswa, yenye misitu minene ya mvua, maziwa yenye maji safi, na wanyama pori wa kipekee. Eneo hili linatoa fursa ya pekee na ya karibu sana ya kukutana na mazingira ya asili, mbali na njia kuu za watalii wa kawaida.

## Hifadhi ya Taifa ya Gombe: Nyumbani kwa Sokwe na Urithi wa Sayansi ya Dunia

Hifadhi ya Taifa ya Gombe ni moja ya maeneo ya kipekee duniani yanayotoa fursa adimu ya kuwaona sokwe wakubwa wakiishi kwa uhuru katika mazingira yao ya asili. Maarufu kimataifa kama "nyumbani kwa sokwe," Gombe ni hazina ya bioanuwai na urithi wa kihistoria, ikijulikana zaidi kwa utafiti wa kisayansi uliofanywa na Dkt. Jane Goodall.

Awali likiwa ni Pori la Akiba tangu mwaka 1943, eneo hili lilipata umaarufu mkubwa duniani mwaka 1960 kupitia utafiti wa sokwe uliofanywa na Dkt. Goodall—utafiti wa muda mrefu zaidi kuwahi kurekodiwa kuhusu jamii ya nyani. Gombe ilipandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1968, na kufunguliwa rasmi kwa utalii mwaka 1978.

Ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 56, hifadhi hii imejipachika kando ya Ziwa Tanganyika, takriban kilomita 16 kutoka mji wa Kigoma. Ndani ya misitu ya Gombe, wageni huweza kuwaona sokwe wa aina mbalimbali, babuni wa mzeituni, na tumbili wa aina tofauti. Hifadhi ya taifa Gombe hutoa fursa ya kupanda milima hadi kwenye maporomoko ya maji yanayo jumuisha Kakombe na Mkenke, vivutio vinavyoongeza haiba ya asili katika eneo hili la kipekee.

Kwa yeyote anayetamani safari ya kipekee yenye historia, sayansi, na asili hai, Gombe ni mahali pa kipekee pasipo na mfano. Ni hazina ya Tanzania na dunia nzima, inayoakisi dhamira ya kweli ya taifa katika kulinda mazingira, uhifadhi wanyamapori, na kuendeleza utafiti wa kisayansi wa kimataifa.



## Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Mahale



Iliyoko kando ya Ziwa Tanganyika, Hifadhi ya Mahale ni mojawapo ya maeneo yenye bioanuwai tajiri zaidi barani Afrika. Msitu wake mnene unaoshuka moja kwa moja hadi kwenye maji safi ya ziwa huifanya Mahale kuwa sehemu bora kwa ufuatiliaji wa sokwe wakubwa na kwa wapenzi wa mandhari ya asili yenye utulivu wa kweli.

Ni mahali ambapo milima hukumbatiana na ziwa, na maisha ya asili hujieleza kwa uzuri wa kupendeza, usioguswa na athari za kisasa. Mandhari yake ni mwaliko wa tafakari, kutulia, na kuungana na roho ya Afrika ya asili.

## Hifadhi za Taifa za Saanane, Rubondo, na Burigi-Chato



Ingawa si maarufu kama hifadhi kubwa, maeneo haya madogo yana uzito wa kipekee kwa watalii wanaotafuta safari za utulivu na ukaribu wa dhati na mazingira ya asili.

Rubondo huwasilisha mandhari adimu ya kisiwa kilichojaa wanyamapori,
Saanane, iliyoko karibu na jiji la Mwanza, ni kivutio rahisi kufikika kinachotoa safari fupi lakini yenye thamani,

Burigi–Chato inajivunia mchanganyiko wa maziwa, savana, na mito, ikiwapa wageni kumbukumbu ya safari ya aina yake.

## Mapori ya Akiba ya Grumeti, Moyowosi, na Kigosi

Maeneo haya ya mbali na yenye utulivu mkubwa ni ngome muhimu za uhifadhi wa wanyamapori na hutoa fursa ya safari za kipekee, hasa katika msimu wa Uhamaji Mkuu wa wanyama. Hapa, wageni hujionea kwa ukaribu mzunguko wa maisha ya porini, katika hali halisi isiyovurugwa na shughuli za kibinadamu.

Kwa ujumla, Kanda ya Magharibi inasalia kuwa miongoni mwa maeneo ya mwisho barani Afrika yaliyo hifadhiwa kwa hali yake ya asili. Mandhari yake safi, bioanuwai ya kipekee, na utulivu wa pori huwapa wageni nafasi ya kushuhudia uzuri wa kweli wa Tanzania—uliojaa uhai, utulivu, na hadhi ya urithi wa dunia. Ni sehemu ambapo Tanzania hujieleza kimya kimya, kwa sauti ya pori na uzuri wa asili usio na kifani.

# Kanda ya Mashariki: Mahali Ambapo Bio-anuai Hukutana na Uzuri wa Pwani

Kanda ya Mashariki ya Tanzania ni mchanganyiko wa kuvutia wa uzuri wa pwani na mandhari ya milima iliyojaa uoto wa asili. Kuanzia misitu ya mikoko hadi milima ya kuvutia ya Udzungwa, eneo hili lenye bioanuwai ya kipekee linajivunia mbuga na hifadhi zinazopatikana kwa urahisi, jambo linalolifanya kuvutia wageni wa ndani na wa kimataifa kwa pamoja.

## Hifadhi ya Taifa ya Saadani:



Hii ndiyo hifadhi pekee nchini Tanzania inayopakana moja kwa moja na Bahari ya Hindi, kiunganishi kwa wanyamapori wa savana na mandhari ya fukwe. Saadani hutoa uzoefu wa kipekee wa safari ya mwituni pembeni ya bahari—safari ya kukumbukwa na ya kipekee duniani.

## *Hifadhi ya Taifa ya Mikumi: Mlango wa Haraka wa Safari ya Asili*



Iko umbali mfupi kutoka Dar es Salaam, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni kivutio maarufu kwa wale wanaotafuta safari ya haraka lakini yenye kusisimua. Ni mahali ambapo wanyamapori wakubwa kama tembo, simba, na mbwa mwitu wanaweza kuonekana kwa ukaribu mkubwa bila ya kulazimika kusafiri kwa umbali mrefu.

Ikiwa katikati ya Tanzania, Mikumi ni hifadhi iliyojaa maisha ya porini. Makundi ya nyati, twiga, pundamilia, tembo na swala huonekana kwa urahisi wakichunga kwa utulivu katika tambarare zake za majani. Twiga huvutia macho ya wageni wakiwa wamesimama kwa haiba wakiila miti ya akasia kando ya Mto Mkata, huku nyumbu na swala pala wakizunguka kwa makundi katika mandhari ya kuvutia.



Mojawapo ya vivutio vya kipekee katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni mabwawa ya viboko, ambayo huwapa wageni fursa ya kuwaona viumbe hawa wakubwa wakiwa majini, wakijitumbukiza na kuibuka kwa mtindo wa kuvutia. Sambamba na hilo, wageni hushuhudia aina mbalimbali za ndege wenye rangi angavu na tabia za kipekee, wanaoifanya Mikumi kuwa chemchemi ya mandhari hai ya asili.

Mikumi ni chaguo bora kwa wasafiri wa ndani na wageni wa kimataifa wanaotamani safari ya karibu na isiyohitaji maandalizi marefu. Hifadhi hii ni uthibitisho halisi wa dhamira ya taifa letu katika kulinda urithi wa mazingira, huku ikiwakaribisha wageni kugusa roho ya pori la Afrika roho iliyojaa uzuri wa asili, utulivu, na maisha ya porini yanayochanua kwa uhuru.

## *Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (zamani Pori la Akiba la Selous):*

Ikiwa mojawapo ya maeneo makubwa zaidi ya hifadhi barani Afrika, Nyerere ni makazi ya wanyama wakubwa kama mamba, viboko, na mbwa mwitu wa Afrika. Safari zake za mtoni zenye mandhari ya kupendeza huwapa wageni fursa ya kuchunguza wanyamapori kwa mtazamo wa kipekee kabisa, wakifurahia mwonekano wa asili wa mito, misitu, na nyasi za savana.

## *Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa:*

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa ni peponi kwa wapandaji milima na wachunguzi wa ndege. Hifadhi hii inatambulika kwa spishi adimu za mimea na wanyama zinazopatikana maeneo haya pekee duniani.

Udzungwa hutoa njia za kupanda milima zilizojaa uoto wa kijani kibichi, maporomoko ya maji ya kuvutia, na hali ya utulivu inayogusa moyo.

Ni kivutio bora kwa wapenzi wa mazingira ya asili wanaotaka kugundua Tanzania ya kweli—iliyohifadhiwa, tulivu, na yenye uzuri wa asili usioguswa.



## *VIVUTIO VYA UTALII VISIWANI ZANZIBAR*

# YAJAYO NI NEEMA TUPU!

# ZANZIBAR YA UCHUMI WA BULUU!!

***Wawekezaji mnakaribishwa kuwekeza nchini kwani bado fursa za uwekezaji ni nyingi hususan utalii wa mikutano na matamasha.***



Zanzibar, kisiwa chenye mandhari ya kuvutia kilichopo pwani ya Tanzania, kinajulikana kwa fukwe zake nzuri za kitropiki, urithi wake tajiri wa kitamaduni, na vivutio vya aina mbalimbali. Miongoni mwa maeneo yanayovutia wageni kwa wingi ni pamoja na Nyumba ya maajabu (House of Wonders); Ngome Kongwe; na Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF) linaloenzi sanaa na utamaduni wa kisiwa hiki.

## Jumba la maajabu (House of Wonders Beit-al-Ajaib)

Likitambuliwa kama jengo refu na maarufu zaidi katika Mji Mkongwe wa Zanzibar, Jumba la Maajabu au Beit-al-Ajaib, ni mojawapo ya alama kuu za kihistoria na utamaduni wa visiwa hivi. Lipo kando ya Barabara ya Mizingani, katikati ya Ngome Kongwe na Makumbusho ya Kasri, likisimama kwa haiba kama mjumbe wa enzi za kale na maendeleo ya karne ya 19.

Jumba hili lilijengwa mwaka 1883 na Sultan Barghash bin Said kama kasri la sherehe na ukumbi wa mapokezi rasmi wa wageni mashuhuri. Kwa wakati wake, lilikuwa alama ya ustawi wa kiutawala na kiteknolojia—ikiwa ni jengo la kwanza Zanzibar kuwa na umeme, na la kwanza Afrika Mashariki kuwa na lifti, hali iliyolipa jina la "Jumba la Maajabu."

Lilibuniwa na mhandisi wa majini kutoka Uingereza na lina sifa ya usanifu wa kisasa wa karne ya 19: varanda pana zilizoshikiliwa na nguzo za chuma, dari refu zinazoruhusu uingizaji hewa wa kutosha, na muundo wa kuvutia uliojengwa kwa mawe ya matumbawe (coral rag), mbao za mikoko, zege, na mihimili ya chuma.

Baadaye, jengo hili lilibadilishwa kuwa Makumbusho ya Historia na Utamaduni wa Zanzibar na Pwani ya Waswahili—mahali ambapo urithi wa kale wa Kiswahili, historia ya biashara ya Bahari ya Hindi, na maendeleo ya jamii ya Waswahili umehifadhiwa kwa uangalifu mkubwa. Hapa ndipo historia ya Afrika Mashariki huishi, ikishuhudia karne nyingi za ustaarabu, biashara, dini, na mahusiano ya kimataifa.



*House of Wonders mwanzoni mwa karne ya 20*



*Jumba la maajabu (House of Wonders)*



## Boma la Kale la Zanzibar

Zanzibar, kisiwa chenye mandhari ya kuvutia kilichopo pwani ya Tanzania, kinajulikana kwa fukwe zake nzuri za kitropiki, urithi wake tajiri wa kitamaduni, na vivutio vya aina mbalimbali. Miongoni mwa maeneo yanayovutia wageni kwa wingi ni pamoja na Nyumba ya maajabu (House of Wonders); Ngome Kongwe; na Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF) linaloenzi sanaa na utamaduni wa kisiwa hiki.

Jengo hili lilijengwa mwaka 1699 na Waarabu kutoka Oman, mara baada ya kuwatimua Wareno waliokuwa wametawala eneo hilo kwa kipindi cha nyuma. Awali, Boma hili lilitumika kama kambi ya kijeshi na gereza na baadae, kati ya mwaka 1905 hadi 1928, lilibadilishwa kuwa kituo cha reli, na mwaka 1947 likawa klabu ya wanawake.

Katika miaka ya 1990, jukwaa la wazi la maigizo (amphitheater) lilijengwa ndani ya boma hili, jambo lililoligeuza kuwa kitovu cha shughuli za sanaa na tamaduni. Kwa sasa, Ngome Kongwe inajumuisha: Uwanja wa ndani wenye maduka ya bidhaa za ukumbusho; Jukwaa la wazi kwa ajili ya maonesho; Mgahawa wa kisasa; na dawati la taarifa kwa watalii.

Ngome hii pia hutumika kama eneo kuu la maonesho na matukio makubwa ya kiutamaduni, likiwa mwenyeji wa matamasha maarufu kama:Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF); na Sauti za Busara, linalosherehekea muziki wa Kiafrika na wa dunia.



*Boma la Kale linavyoonekana kutoka Jumba la Maajabu*

## Mji Mkongwe Wa Zanzibar – Urithi wa Dunia

Mji Mkongwe wa Zanzibar, uliotambuliwa rasmi na UNESCO kama Urithi wa Dunia, ndio moyo wa utamaduni wa visiwa vya Zanzibar, ukiwa umejikita katika Kisiwa cha Unguja. Jina lake linatokana na usanifu wa kipekee wa majengo ya karne ya 19, unaoonesha mchanganyiko wa athari za Kizungu, Kiarabu, Kihindi na Kiswahili—ambazo kwa pamoja zinashuhudia historia ya mwingiliano wa tamaduni mbalimbali katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

Kwa upande wa kihistoria, Mji Mkongwe ulikuwa kitovu kikuu cha biashara ya kimataifa, ukiwavutia wafanyabiashara kutoka bara la Afrika, Asia na Ulaya. Biashara ya karafuu, dhahabu, pembe za ndovu, pamoja na biashara ya watumwa, vilifanyika kwa wingi katika bandari na sokoni mwa mji huu wa kihistoria.

Leo hii, Mji Mkongwe unaendelea kuvutia kwa: Mitaa yake myembamba yenye mwonekano wa kale; Masoko ya kienyeji yaliyojaa harufu na rangi za viungo vya asili; Misikiti ya kihistoria na; Majengo yaliyosimama kwa haiba ya kihistoria.

Vivutio vikuu vya kihistoria vinavyopatikana Mji Mkongwe ni pamoja na:

- Kanisa Kuu la Anglikana – lililojengwa mahali palipokuwa soko la watumwa;
- Jumba la Sherehe (The Palace Museum) – lililokuwa makazi ya kifalme ya Sultani;
- Mabafu ya Kidichi – mabafu ya kifalme ya Kiajemi yaliyojengwa na Sultani kwa ajili ya malkia wake wa Kifarsi;
- Magofu ya Dunga – yaliyobeba historia ya utawala wa Kiarabu visiwani;
- Jumba la Kumbukumbu la Amani; na
- Makaburi ya Makusurani – ambako wamelazwa watawala wa Kiarabu wa enzi za Sultani.



*Muonekano kutoka angani wa Mji Mkongwe, katika Kisiwa cha Unguja*

## Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF)

Likitambulika pia kama Tamasha la Nchi za Dau, ZIFF ni miongoni mwa matukio makubwa zaidi ya kitamaduni katika ukanda wa Afrika Mashariki, likifanyika kila mwaka visiwani Zanzibar, Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997, tamasha hili limekuwa jukwaa muhimu la kuhamasisha sanaa ya filamu, urithi wa kitamaduni, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia nguvu ya ubunifu.

Tamasha hili la siku kumi hujumuisha:

- Maonyesho ya filamu kutoka Afrika na mataifa ya kimataifa;
- Warsha za kitaalamu kwa wasanii na waandaaji filamu;
- Mijadala ya kielimu kuhusu masuala ya kijamii, sanaa, na tamaduni;
- Maonesho ya muziki ya kila usiku; na
- Shughuli za mitandao ya ushirikiano wa kimataifa

Filamu huonyeshwa katika maeneo ya kihistoria ya Mji Mkongwe pamoja na vijijini, ili kuwafikia watu wa tabaka na maeneo tofauti, na hivyo kuendeleza ushiriki wa jamii kwa upana.

## Programu za Kijamii za ZIFF

Mbali na filamu, ZIFF huendesha pia programu za kijamii zenye kugusa maisha ya watu moja kwa moja, zikiwemo:

- Kambi za Ujuzi wa Maisha kwa Watoto kwa kushirikiana na UNICEF;
- Kambi za Amani kwa Watoto zinazolenga kueneza ujumbe wa amani na mshikamano;
- Ziara za Kihistoria na Kiutamaduni katika vijiji mbalimbali vya Zanzibar;
- Programu hizi huongeza thamani ya tamasha hilo kwa kulenga maendeleo ya watu, hasa watoto na vijana.



# *Fukwe za Zanzibar – Urithi wa Asili na Kivutio cha Dunia*

Zanzibar inajivunia kuwa na baadhi ya fukwe nzuri zaidi duniani, kila moja ikiwa na mandhari ya kipekee na inayowapa wageni kumbukumbu ya kipekee. Fukwe za upande wa magharibi zinajulikana kwa machweo ya jua yenye kuvutia, huku pwani ya kusini ikiwa maarufu kwa uwepo wa pomboo wanaoonekana kwa urahisi katika maji ya kina kifupi.



**Miongoni mwa fukwe maarufu zaidi ni:**

**Fukwe za Nungwi** – zenye mchanga mweupe wa kuvutia na maji ya rangi ya samawati, eneo hili limekuwa kitovu cha utalii wa kimataifa. Wageni hufurahia hoteli za kisasa, baa, burudani za usiku, na mandhari ya kupendeza.



**Fukwe za Kendwa** – zinazovutia kwa shamrashamra za usiku na hali ya hewa tulivu, Kendwa ni chaguo maarufu kwa wasafiri wanaotafuta maisha ya furaha na starehe kando ya bahari.

**Fukwe za Paje** – maarufu kwa shughuli za kuogelea, kupiga mbizi, na michezo ya baharini kama kite surfing. Eneo hili linapendwa na wapenda maumbile na wasanii wa picha.



Fukwe hizi si tu vivutio vya utalii, bali pia ni sehemu ya urithi wa asili unaoendeleza ustawi wa jamii za pwani na kuchangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa visiwa vya Zanzibar. Mandhari yake ya kuvutia, pamoja na utamaduni wa kipekee wa watu wa pwani, huwapa wageni kila sababu ya kurudi tena.

## *Shughuli za Fukwe Zanzibar: Upekee na Burudani kwa Kila Mgeni*

Wageni wanaotembelea Zanzibar wana nafasi ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuvutia na za kimataifa kwenye fukwe zake maridadi. Miongoni mwa shughuli maarufu zinazopatikana ni kupiga mbizi kwa kutumia vifaa (snorkeling), mbizi za kina kirefu (scuba diving), kurusha upepo kwa ubao (windsurfing), kuruka angani kwa parachuti ya kuvutwa na boti (parasailing), pamoja na kuendesha pikipiki za matairi manne (quad biking) katika njia za mchanga na pwani.
Pia, kuna safari maalum za jioni baharini kwa kutumia madau ya kitamaduni, maarufu sana kwa mtazamo wa machweo ya jua katika anga ya Bahari ya Hindi uzoefu unaobeba utulivu na uzuri wa visiwa hivi.

Ili wageni waweze kufurahia kwa urahisi uzuri wa fukwe mbalimbali, inashauriwa kuchagua hoteli zilizopo katika maeneo yenye miundombinu bora ya usafiri. Ni muhimu kutambua kuwa fukwe zote za Zanzibar ni za umma na hazitozwi kiingilio — hivyo kila mtu anakaribishwa kufurahia utajiri wa asili wa visiwa hivi.





# SEHEMU
## YA SITA

06

### SEHEMU YA SITA: FURSA ZA UWEKEZAJI TANZANIA

- Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo (Uvuvi, Mifugo na Misitu)
- Uwekezaji katika Sekta ya Utalii
- Uwekezaji katika Sekta ya Viwanda
- Uwekezaji katika sekta ya ujenzi na mali isiyohamishika
- Uwekezaji katika Sekta ya Madini
- Uwekezaji katika uchumi wa Buluu
- Uwekezaji katika sekta ya michezo na ubunifu
- Uwekezaji katika sekta ya huduma za kifedha
- Uwekezaji katika sekta ya huduma

Tanzania ni nchi yenye fursa nyingi za uwekezaji kwa raia wake pamoja na wageni kutoka nje ya nchi. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imeainisha sekta 9 za kimkakati zenye uwezo mkubwa wa kuchochea mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Dira imeweka msingi thabiti wa vigezo vya kutambua sekta zitakazochangia ukuaji wa uchumi na kutoa fursa nyingi za ajira. Hivyo wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi wazian-galie zekta hizi kama fursa ya kufika maendeleo na uwekezaji endelevu. Sekta hizi ni kama ifuatavyo:

# 1. Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo (Uvuvi, Mifugo na Misitu)

Sekta ya kilimo bado bado ni mhimili wa uchumi wa Tanzania, kikichangia asilimia 26.5 ya pato la Taifa, ikiajiri asilimia 65 ya nguvukazi, na kuzalisha asilimia 30 ya mapato ya mauzo ya nje. Tanzania ina jumla ya hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo, ambapo hekta milioni 29.4 zinaweza kumwagiliwa maji. Sekta hii ina uwezo wa kuzalisha ajira nyingi na kuchochea ongezeko la mapato kupitia mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani. Uhusiano wake na sekta za viwanda, usafirishaji, na biashara unabainisha nafasi yake katika kukuza ajira na uchumi.

Tanzania ni nchi yenye mifugo mingi ikishikilia nafasi ya pili kwa uwingi wa mifugo barani Afrika, lakini chini ya asilimia 1 ya nyama inachakatwa nchini. Tanzania pia huzalisha tani 300,000 za sukari kwa mwaka, lakini kuna pengo la tani 220,000 linalokua kwa asilimia 6 kila mwaka. Hali ya hewa na udongo wa Tanzania vinafaa sana kwa kilimo cha miwa na eneo lina uwezo mkubwa wa umwagiliaji.

Tanzania ina pwani yenye urefu wa kilomita 1,424 katika Bahari ya Hindi na ina vyanzo vikubwa vya maji baridi. Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazozalisha samaki kwa wingi barani Afrika na inashika nafasi ya juu ya 10 barani kwa uzalishaji wa samaki. Sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.4 ya Pato la Taifa na asilimia 10 ya mapato ya fedha za kigeni, huku ikizalisha tani 341,065 za samaki kila mwaka. Zaidi ya wavuvi 177,000 huitegemea moja kwa moja, na watu milioni 4 hutegemea uvuvi kama chanzo cha maisha.

Uwekezaji katika sekta ya kilimo unatoa fursa kwa wawekezaji wazawa, diaspora na wawekezaji wakigeni kuchangia kwenye ukuaji wa sekta hii, kuleta mageuzi kwenye ukuaji wa pato la taifa na kusaidia kwenye kupambana na tatizo la ukosefu wa ajili na zaidi ya yote, kutoa nafasi ya kutengeneza faida kubwa kutokana na uwekezaji wao.

# 2. Uwekezaji katika Sekta ya Utalii



Sekta ya utalii Tanzania inachangia asilimia 25 ya mapato ya mauzo ya nje ya Tanzania na ni mojawapo ya sekta kuu za uchumi. Sekta hii ina mchango muhimu katika kuimarisha urari wa malipo na kuchochea ukuaji wa pato la Taifa. Utalii unaendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya fedha za kigeni, ukichochea sekta muhimu kama vile za ukarimu, usafiri na biashara. Sekta hii inakua kwa kasi, ikichangia asilimia 17.2 ya Pato la Taifa (GDP).

Watalii hukaa nchini kwa wastani wa siku 10–11, wakitumia takriban dola za Kimarekani 355 kwa matembezi ya kifurushi na dola 247 kwa matembezi yasiyo ya kifurushi. Kwa kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za malazi na utalii wa kipekee, Tanzania inajitokeza kuwa soko la kuvutia kwa uwekezaji katika hoteli, ekoturizimu, na huduma nyingine za utalii na uwekezaji katika sekta hii una tija kubwa kwa wawekezaji na kwa sekta husika.

# 3. Uwekezaji katika Sekta ya Viwanda



Sekta ya viwanda nchini Tanzania bado iko hatua za awali lakini inaendelea kukua kwa kasi ya asilimia 8.3 kwa mwaka na kuchangia asilimia 8.1 ya Pato la Taifa. Sekta hii inaajiri takriban watu 306,180 na huchangia asilimia 18.1 ya fedha za kigeni kupitia kodi na biashara.

Uwekezaji katika sekta ya viwanda una fursa nyingi kutokana na utegemezi mkubwa wa bidhaa zinazoagizwa nje kama bidhaa za magari, pengo la tani 220,000 za sukari, na uagizaji wa asilimia 60 ya mafuta ya kula. Vilevile, upatikanaji wa gesi asilia na madini unatoa fursa ya uzalishaji wa bidhaa nchini. Sekta hii pia ni ya kuvutia kwa makampuni ya bidhaa za chakula na vinywaji.

Kuelekea mwaka 2050, sekta ya ujenzi inatarajiwa kukua kwa kasi, ikizalisha mamilioni ya ajira katika nyanja za ujenzi, usanifu, uhandisi na kazi za ustadi. Ukuaji huu utachochea mapato na kuimarisha maendeleo ya miji yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za kisasa. Sekta hizi mbili zitafungamana na sekta za viwanda na huduma kama vile usimamizi wa mali na huduma za sheria. Ukuaji endelevu wasekta hizi utatokana na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya kisasa, ujenzi wa makazi nafuu, na mbinu endelevu za ujenzi.

# 4. Uwekezaji katika sekta ya ujenzi na mali isiyohamishika

Sekta ya majengo nchini Tanzania ni eneo lenye fursa kubwa ya uwekezaji, hasa katika miji inayokua kwa kasi kama Dar es Salaam na Dodoma. Mahitaji yanayoongezeka ya makazi na majengo ya kibiashara yanasukumwa na ukuaji wa uchumi, ongezeko la idadi ya watu (zaidi ya milioni 60, ikiendelea kukua kwa asilimia 2.7 kila mwaka), pamoja na uamuzi wa serikali kuhamishia makao makuu yake Dodoma.

Ili kukabiliana na uhaba wa nyumba, wawekezaji wanahamasishwa kushirikiana na mashirika ya kitaifa kama Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), au kampuni binafsi, katika kujenga makazi ya kisasa, ofisi na hoteli katika maeneo mbalimbali ya nchi.



# 5. Uwekezaji katika Sekta ya Madini




Sekta ya madini ni mhimili muhimu wa uchumi wa Tanzania, ikichangia pakubwa katika mapato ya fedha za kigeni. Sekta hii ina aina mbalimbali za shughuli kuanzia kampuni kubwa, zile za kati hadi wachimbaji wadogo.

Tanzania ina rasilimali nyingi za madini kama vile makaa ya mawe, shaba, almasi, dhahabu, nikeli, fedha, urani, na vito adimu vya Tanzanite vinavyopatikana sehemu moja tu duniani. Huku kukiwa na ugunduzi wa gesi asilia kwa wingi, serikali ina mpango wa kutumia pia mitambo ya makaa ya mawe kutatua changamoto za upatikanaji wa nishati.

Fursa muhimu za uwekezaji ni pamoja na uchenjuaji wa madini ya thamani, usafishaji wa vito, uanzishaji wa kiwanda cha kuzalisha soda kaustiki (caustic soda) Engaruka, uzalishaji wa chuma na bati Liganga, uchakataji wa nikeli Kabanga, na uchimbaji wa urani Mkuju. Uwekezaji katika mitambo ya kuyeyusha madini ni fursa nyingine yenye matumaini makubwa na yenye kusaidia kukuza sekta ya viwanda nchini.

# 6. Uwekezaji katika uchumi wa Buluu



Uwekezaji katika sekta ya uchumi buluu unaozingatia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na maji baridi, utakuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo nchini. Tanzania, ambayo ina ukanda mrefu wa pwani, maziwa na mito mikubwa, ina fursa nyingi za kukuza sekta za uvuvi, utalii wa pwani na wa maziwa, usafiri wa majini, na matumizi ya nishati mbadala kutoka baharini. Sekta hizi zina nafasi kubwa ya kuongeza ajira, kukuza mapato, na kuhifadhi mazingira. Ili nchi iweze kutumia fursa hizi kikamilifu, itakuwa muhimu kuwekeza katika gesi asilia, uhifadhi wa bahari, uvuvi endelevu na ujenzi wa miundombinu. Hatua za kimkakati katika gesi asilia, uendelezaji wa bandari na upanuzi wa nishati ya kutumia maji zitachangia mpango madhubuti wa kutumia kikamilifu fursa za uchumi wa buluu Tanzania.

## 7. Uwekezaji katika sekta ya michezo na ubunifu

Sekta hii ina uwezo mkubwa ambao haujatumiwa kikamilifu katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Sekta hizi zinatoa fursa muhimu za ajira, kuendeleza ujuzi, kuwa chanzo cha kipato na kuwawezesha vijana, wakati huo huo zikijenga umoja na mshikamano wa jamii. Tanzania inalenga kuwa kitovu cha utamaduni, sanaa bunifu na michezo barani Afrika ifikapo mwaka 2050, ikiwa na sekta zinazostawi katika muziki, filamu, mitindo, na burudani. Kwa kukuza vipaji na kuweka mazingira wezeshi, Tanzania itafungua milango ya ubunifu na ujasiriamali kwa vijana. Kadhalika, uwekezaji kwenye mifumo ya haki za uvumbuzi utakuwa muhimu ili kuhakikisha kwamba sekta hizi zinashamiri na kuwa endelevu.



# 8. Uwekezaji katika sekta ya huduma za kifedha

Mahitaji ya huduma za kifedha, bima na uwekezaji yatakua kwa kiasi kikubwa kutokana na ongezeko la watu na ukuaji wa miji. Huduma bora za kifedha zitaimarisha upatikanaji wa mikopo, kukuza uwekezaji, kuweka akiba, na kuimarisha mbinu za ujasiriamali na hivyo kurasimisha shughuli za kiuchumi. Uwekezaji katika sekta hii kutaimarisha mifumo rasmi ya kifedha na upatikanaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya wajasiriamali na wawekazaji katika viwanda vidogo na vya kati wanaokosa mikopo kutoka vyanzo rasmi.




# 9. Uwekezaji katika sekta ya huduma

Sekta ya huduma ina nafasi muhimu katika kuendesha maendeleo ya Tanzania, hususan katika maeneo ya biashara, huduma za ukarimu, na huduma nyingine za kijamii na kiuchumi. Kuongezeka kwa watu walio na kipato cha kati kutaongeza mahitaji ya bidhaa na huduma, hivyo kuchochea ajira, kupanua fursa za biashara na kuimarisha shughuli za kiuchumi. Uwekezaji katika sekta hii utasaidia ukuaji wa sekta hii na kuengea tija ya uwekezaji kwa wawekaji kwa kipindi kirefu.



07

# SEHEMU YA SABA

## FURSA ZA ELIMU ZINAZOPATIKANA JAMHURI YA WATU WA CHINA KUPITIA USHIRIKIANO KATI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) NA CHAMA CHA KIKOMUNISTI CHA CHINA (CPC)

- *Fursa za kujifunza Lugha ya Kichina nchini Tanzania na China*
- *Fursa za Ufadhili wa masomo kwa watanzania nchini china*



Uhusiano kati ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China ni wa kihistoria, ukijengwa juu ya misingi ya mshikamano, kuheshimiana, na kusaidiana. Tangu enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na Kiongozi wa China wa wakati huo, Mwenyekiti Mao Zedong, urafiki huu umekuwa ukistawi katika nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni.

Miongoni mwa nguzo muhimu zinazouimarisha uhusiano huu wa kidugu ni elimu. Kupitia elimu yenye viwango vya kimataifa inayotolewa chini ya usaidizi wa China, vijana wa Tanzania wameendelea kupata uelewa mpana wa masuala ya siasa, uchumi, utawala bora, pamoja na maendeleo ya teknolojia.

Ushirikiano wa karibu kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) umeimarisha mazingira ya ushirikiano wa kisiasa na kijamii. Kupitia makubaliano haya ya kirafiki, fursa nyingi za elimu zimefunguka kwa Watanzania, ikiwa ni pamoja na programu za kubadilishana wanafunzi, mafunzo ya muda mfupi kwa wataalamu wa fani mbalimbali, na udhamini wa masomo ya muda mrefu kwa ngazi mbalimbali za elimu ya juu.

Sisi, wanachama wa Tawi la CCM nchini China, kupitia kamati ya maandalizi ya jarida hili, tumeandaa muongozo wa kina na wa vitendo utakaomwezesha kila kijana au raia wa Tanzania aliye na shauku ya kusoma nchini China kufahamu hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kupata fursa hiyo.

# *(I) Fursa za Kujifunza Lugha ya Kichina Nchini Tanzania na China.*

## *1. Taasisi Zinazo Fundisha Lugha ya Kichina Nchini Tanzania*

Katika jitihada za kuimarisha uhusiano wa utamaduni, diplomasia, na biashara kati ya Tanzania na China, lugha ya Kichina (Mandarin) imechukua nafasi muhimu kama lugha ya kimataifa ya mawasiliano.

Ili kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia, biashara, na utamaduni kati ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China, taasisi mbalimbali za elimu nchini Tanzania zimeanzisha programu rasmi za kufundisha lugha ya Kichina (Mandarin) kwa Watanzania. Taasisi hizi hutoa mafunzo kwa wanafunzi wa shule na vyuo, wataalamu wa fani mbalimbali, pamoja na maafisa wa serikali. Mafunzo hayo yamekuwa daraja muhimu la kuimarisha biashara za kimataifa, uamuzi wa kisera, na maelewano ya kiutamaduni baina ya mataifa haya mawili.

Kwa kupitia lugha, Watanzania wanapata fursa ya kufahamu mfumo wa kijamii na kiuchumi wa China, jambo ambalo limeongeza nafasi ya ushiriki wao katika miradi ya pamoja, biashara ya kimataifa, na ufuatiliaji wa programu za maendeleo zinazo-

fadhiliwa na Serikali ya China. Baadhi ya taasisi hizo zimeorodheshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1: Taasisi zinazotoa mafunzo ya lugha ya kichina Tanzania**

| Na | JINA LA TAASISI | ANUANI/LINK |
|---|---|---|
| 1 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) – Taasisi ya Confucius | https://www.udsm.ac.tz/confucius-institute |
| 2 | Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) – Idara ya Lugha ya Kichina | https://www.udom.ac.tz/academic_unit/index?id=VFZSUlBRPT0= |
| 3 | Taasisi ya Confucius – Chuo Kikuu cha Zhejiang Normal (Mpango wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China) | https://iczu.zju.edu.cn/iczuen/wonfuciuswwnstitute/list.htm |

## 2. Taasisi Zinazofundisha Lugha ya Kiswahili Nchini China

Kwa upande mwingine, China imetambua lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha ya kimkakati barani Afrika, hasa kwa mataifa ya Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika. Kutokana na nafasi hiyo, baadhi ya vyuo vikuu vya China vimeanzisha programu rasmi za kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Kichina, watafiti, na wanadiplomasia.

Hatua hii inalenga kuandaa wataalamu wa lugha na tafsiri, kurahisisha shughuli za kibalozi na kibiashara kati ya China na nchi zinazozungumza Kiswahili, pamoja na kukuza uelewa wa kina kuhusu historia, jamii, na tamaduni za Afrika. Baadhi ya vyuo vinavyofundisha lugha ya kiswahili nchini China vimeorodheshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2: Vyuo vinavyofundisha lugha ya Kiswahili nchini China**

| Na | JINA LA TAASISI | ANUANI/LINK |
|---|---|---|
| 1 | Chuo Kikuu cha Mafunzo ya Lugha za Kigeni cha Beijing (BFSU) – Idara ya Kiswahili | https://en.bfsu.edu.cn/2021/08/20/c_158215.htm |
| 2 | Chuo Kikuu cha Zhejiang Normal (ZJNU) – Mpango wa Lugha ya Kiswahili | https://iczu.zju.edu.cn/iczuen/wonfuciuswwnstitute/list.htm |
| 3 | Chuo Kikuu cha Mafunzo ya Lugha za Kigeni cha Guangdong – Kozi za Kiswahili | https://gdufs.cucas.cn/ |

| Na | JINA LA TAASISI | ANUANI/LINK |
|---|---|---|
| 4 | Chuo Kikuu cha Mafunzo ya Kigeni cha Tianjin | http://tjfsu.admissions.cn/course/view/19068-Swahili |

Vyuo hivi hutoa masomo ya Kiswahili kwa ngazi mbalimbali: kuanzia stashahada hadi digrii ya kwanza na ya pili, pamoja na kozi fupi za muda kwa watumishi wa serikali, wanadiplomasia na wanafunzi wa kimataifa. Mpango huu wa kufundisha lugha ya Kichina na Kiswahili katika taasisi za elimu ya juu nchini Tanzania na China unachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza elimu na tamaduni zetu kwa kuweka msingi thabiti ya kitaaluma baina ya mataifa haya mawili.

### *Mpango wa Kufundishana Lugha kati ya Tanzania na China: Nguzo ya Kukuza Elimu na Ustaarabu wa Pande Mbili*

Vyuo hivi hutoa masomo ya Kiswahili kwa ngazi mbalimbali: kuanzia stashahada hadi digrii ya kwanza na ya pili, pamoja na kozi fupi za muda kwa watumishi wa serikali, wanadiplomasia na wanafunzi wa kimataifa. Mpango huu wa kufundisha lugha ya Kichina na Kiswahili katika taasisi za elimu ya juu nchini Tanzania na China unachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza elimu na tamaduni zetu kwa kuweka msingi thabiti ya kitaaluma baina ya mataifa haya mawili.

Mpango huu umechangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza elimu na tamaduni zetu, huku ukijenga daraja la maarifa, uelewa wa kidiplomasia, na fursa za kitaaluma kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kupitia ushirikiano huu, wasomi wa Kitanzania wameweza kushiriki kikamilifu katika mijadala ya kitaaluma, kisiasa, na kiuchumi nchini China, na hivyo kuimarisha sauti ya Tanzania katika majukwaa ya kimataifa. Aidha, lugha imekuwa chombo muhimu cha ushawishi na ujenzi wa nafasi ya Tanzania katika masuala ya kikanda na kimataifa.

## *(II) Fursa za Ufadhili wa Masomo kwa Watanzania Nchini China*

### *1. Programu za Ufadhili Zinazopatikana*

Kupitia ushirikiano kati ya Tanzania na China, Watanzania wana fursa ya kuomba ufadhili wa masomo kamili au wa sehemu kwa ngazi ya shahada ya kwanza (undergraduate), shahada ya uzamili (master's), na shahada ya uzamivu (PhD). Programu hizi zimewajengea vijana uwezo wa kitaaluma katika ujuzi wao.

**(a) Ufadhili wa Serikali ya China (CSC Scholarships)**

Ufadhili huu unaratibiwa na Wizara ya Elimu ya China ikihusisha mambo yafuatayo:

**Jedwali 3: Aina za ufadhili zinazotolewa na serikali ya China (Ufadhili wa CSC)**

| Na | AINA YA UFADHILI WA CSC | ANUANI/LINK |
|---|---|---|
| 1 | Mpango wa Nchi Mbili (Bilateral Program) – Hutoa ufadhili kupitia makubaliano rasmi kati ya Tanzania na China. | https://www.csc.edu.cn/ https://www.chinesescholarshipcouncil.com/ https://studyinchina.csc.edu.cn/#/login |
| 2 | Mpango wa Vyuo vya China (Chinese University Program) – Ufadhili unaotolewa moja kwa moja na vyuo vikuu | |
| 3 | Mpango wa Great Wall – Ufadhili maalum kwa wanafunzi kutoka nchi zinazoendelea. | |

**Zingatia:** Ufadhili wa CSC ni wa aina tofauti. Wanafunzi wanashauriwa kusoma kwa makini masharti na vigezo vya kila aina ya ufadhili kabla ya kuomba.

**(b) Ufadhili wa MOFCOM (Wizara ya Biashara ya China)**

Aina hii ya ufadhili hutolewa na Wizara ya Biashara ya Jamhuri ya Watu wa China (MOFCOM) kwa ajili ya wanafunzi wa shahada ya uzamili (Master's) na shahada ya uzamivu (PhD), hususan katika fani zinazolenga maendeleo ya moja kwa moja ya taifa la Tanzania, kama vile: Uchumi na Biashara; Uhandisi na Teknolojia; na Sera za Umma na Utawala Bora.

Ufadhili huu ni kamili na huhusisha ada ya masomo, malazi, bima ya afya, posho ya kila mwezi, na nauli ya ndege ya kwenda na kurudi. Lengo kuu ni kuwajengea uwezo wataalamu kutoka nchi zinazoendelea ili kuleta ufanisi katika taasisi za serikali na sekta binafsi.

Kwa kawaida, tangazo la nafasi hutolewa kila mwaka kati ya mwezi Machi hadi Mei, ambapo uratibu wa mchakato hufanywa kwa ushirikiano kati ya Ubalozi wa China nchini Tanzania na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Waombaji wote wanashauriwa kufuatilia matangazo rasmi kupitia:

- Tovuti ya Ofisi ya Rais – Utumishi - https://www.utumishi.go.tz/documents/scolarships
- Tovuti ya MOFCOM Scholarships – China Scholar https://www.china-scholar.com/scholarships/mofcom-scholarships-china/

Maombi rasmi yanapaswa kufanywa kupitia njia zilizotangazwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waombaji hawatakiwi kuwasilisha maombi moja kwa moja kwa chuo kabla ya maelekezo rasmi kutolewa.

**(c) Ufadhili wa Serikali za Mitaa na Vyuo Vikuu vya China**

Mbali na ufadhili wa serikali kuu ya China, mikoa na majiji mbalimbali nchini humo hutoa pia ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kimataifa kwa lengo la kuhamasisha ushirikiano wa kimataifa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu.

**Jedwali 4: Ufadhili wa Serikali za Mitaa na Vyuo Vikuu vya China**

| Na | AINA YA UFADHILI WA CSC | ANUANI/LINK |
|---|---|---|
| 1 | Ufadhili wa Mji wa Zhejiang – Hutolewa na vyuo kama Zhejiang University of Science and Technology, na Zhejiang Normal University. | https://www.cucas.cn/school_redirect/schoollist |
| 2 | Ufadhili wa Serikali ya Jiji la Shanghai – Mfano: East China Normal University. | |
| 3 | Mpango wa Great Wall – Ufadhili maalum kwa wanafunzi kutoka nchi zinazoendelea. | |

## 2. Jinsi ya Kuomba Ufadhili wa Masomo nchini China

**Hatua ya 1: Kusanya Nyaraka Muhimu**

Kabla ya kuanza mchakato wa maombi, hakikisha umekusanya nyaraka zifuatazo:

i). Pasipoti halali ya Kitanzania (kupatikana kupitia Immigration Tanzania – Huduma za Pasipoti)

ii). Vyeti vya kuhitimu masomo ya awali kwa ngazi husika

iii). Fomu ya uchunguzi wa afya, iliyojazwa kikamilifu na kugongwa muhuri wa daktari

iv). Cheti cha kutothibitisha makosa ya jinai (Police Clearance)

v). Cheti cha ujuzi wa lugha ya Kiingereza (TOEFL/IELTS) endapo kinahitajika

vi). Barua tatu za mapendekezo kutoka kwa maprofesa, waajiri, au maafisa wa serikali

vii). Mpango wa masomo au pendekezo la utafiti (kwa waombaji wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu)

viii). Barua ya motisha na wasifu binafsi (CV)

**Hatua ya 2: Tuma Maombi Kupitia Majukwaa Rasmi ya Mtandaoni**

i) .Kwa Ufadhili wa Serikali ya China (CGS/CSC): Tembelea CSC Application Portal kupitia: https://www.campuschina.org

ii) .Kwa Ufadhili wa MOFCOM (Wizara ya Biashara ya China): Fuata maelekezo rasmi kupitia jukwaa la MOFCOM Scholarship

iii) .Kwa Maombi ya Moja kwa Moja Vyuo Vikuu: Baadhi ya vyuo hutaka barua ya kukubalika awali (Pre-admission Letter) kabla ya kuendelea na mchakato wa ufadhili.

**Hatua ya 3: Fuatilia kupitia ubalozi wa China nchini Tanzania**

Ubalozi wa China nchini Tanzania hutoa usaidizi wa kimkakati, uthibitisho wa nyaraka, na mwongozo wa hatua kwa hatua za mchakato wa maombi.

**Hatua ya 4: Fuatilia maendeleo ya maombi yako**

Tembelea mara kwa mara jukwaa la maombi, angalia barua pepe yako kwa taarifa au mabadiliko muhimu kuhusu maombi yako ya ufadhili.

**Kwa Taarifa Zaidi, Tembelea:**


- Wizara ya Mambo ya Nje ya China (PRC): https://www.fmprc.gov.cn/mfa_eng/
- Kituo cha Ushirikiano wa Lugha na Elimu: http://www.chinese.cn/page/#/pcpage/mainpage
- CSC Scholarship Portal (campuschina.org): https://www.campuschina.org/index.html
- Wizara ya Elimu ya China: http://en.moe.gov.cn/
- Taasisi za Lugha ya Kichina Nchini Tanzania:

  UDSM Confucius Institute: https://www.udsm.ac.tz/confucius-institute

  UDOM Chinese Department: https://www.udom.ac.tz/academic_unit/index?id=VFZSUlBRPT0=

  Zhejiang Normal University Confucius Program: https://iczu.zju.edu.cn/iczuen/wonfuciuswwnstitute/list.htm

- Ofisi ya Rais – Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Scholarship Updates): https://www.utumishi.go.tz/documents/scolarships


CHAMA CHA MAPINDUZI
MWISHO